SUPA JACKPOT
TZS. 1,120,448,224
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Viongozi** wa dini: Talaka zisitolewe mahakamani, tuachieni

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Mei 31, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581327
www.ippmedia.com
The Citizen digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Bangi katika biskuti, keki

• **Uchunguzi** wabaini pia imo ndani ya majani ya chai, kahawa, juisi, asali... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**TANESCO YASEMA SGR HAITOKOSA UMEME**
SHIRIKA la Umeme Tanzania...

UKURASA WA 4
**ACT-WAZALENDO YALIA NA UMASKINI RUKWA**
CHAMA cha ACT-Wazalendo...

UKURASA WA 5
**CHONGOLO ATAKA USIMAMIZI SKIMU**
KATIBU Mkuu wa Chama Cha....




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea kijarida chenye maelezo kuhusu matumizi ya nishati mbadala ya kupikia kutoka kwa Waziri wa Nishati, January Makamba, alipofungua maonyesho ya Wiki ya Nishati, viwanja vya Bunge mjini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Biden ang'aka sheria ushoga Uganda

UKURASA 19



## Dk. Mwinyi asisitiza hawatoficha kitu Ripoti ya CAG Z'bar

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YATUMA 'MASHUSHUSHU' ALGERIA UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Bangi yawekwa katika chakula

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBINU mpya ya kusambazwa na kutumiwa kwa dawa za kulevya aina ya bangi imebainika kutokana na kuwekwa katika baadhi ya vyakula na vinywaji kama chai, keki, biskuti, juisi na asali.

Mbinu hizo zimegundulika kutokana na jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, bangi ikiwamo, huku onyo likiendelea kutolewa dhidi ya wanaotumia kilevi hicho haramu na kuweka katika vyakula na vinywaji.

Aidha, kubainika huko kumeifanya serikali kutangaza operesheni kwenye viwanda vya kutengeneza vyakula na vinywaji ikiwa ni sehemu ya mapambanio dhidi ya dawa za kulevya.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasilisha bungeni taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2022 iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Alisema baada ya kufanya utafiti na kugundua tatizo, walikubaliana kufanya operesheni maalum za kujua maeneo na ukamataji ukazaa matunda katika baadhi ya mikoa ikiwamo ya Kilimanjaro na Arusha.

"Kuna dada Arusha na mume wake raia wa kigeni, tulikuta wanatengeneza bidhaa zikiwamo biskuti, keki na asali zote zimewekwa bangi kwa kilevi kikubwa zimeshafungwa kwa ajili ya kupelekwa nje ya nchi. Wameshafungwa miaka 30 jela na hii ndiyo fundisho kwa wote," alisema.

Pia alisema katika operesheni zao wamekutana na kiwanda kimoja (jina hakulitaja) ambacho kinazalisha biskuti ambazo zinatengenezwa kwa kuchanganywa na bangi.

Alisema wamegundua kwamba kuna ulimaji wa aina mbili wa bangi na kwa maana ya ile inayozalisha kama zao la biashara na kusafirisha kwenye masoko nje kama Arusha, Iringa, Morogoro, Manyara wakati Mara na Ruvuma inazalisha kwa matumizi ya ndani.

"Hivi karibuni kumeibuka tabia ya kuchanganya bangi yenye kiasi kikubwa chenye kilevi kwenye vyakula kama biskuti, asali, juisi, majani ya chai na wakati mwingine mpaka keki," alisema.

Waziri alisema katika mapambano dhidi ya dawa hizo za kulevya, mwaka 2022 serikali iliteketeza ekari 179 za mashamba ya bangi na tani 20.58 za dawa hiyo zilikamatwa.

Alisema kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo wamekubaliana kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ukiwamo mkoa wa Arusha eneo la Kisimiu Juu kuangalia wanaoongoza kwa kilimo cha bangi, wanakilima kibiashara ili kusaidia kupata mazao mbadala ya kujiingizia kipato.

"Tutafanya utafiti kujua ni mazao gani yanakubali maeneo hayo wanakilima bangi tunaamini vijana wataondoka huko na kurudi kwenye mazao mbadala.

"Haya mabadiliko ya kitabia na mwenendo mzima wa matumizi ya dawa za kulevya ni lazima tuwe tunahabarishana Watanzania, kama kuna Mtanzania ataona kuna chakula ambacho hakielewi atoe taarifa, mamlaka tumeipa nguvu ya kifedha na kimamlaka katika kupambana," alisema.

Sambamba na hilo, alisema kuna taarifa nyingi kwenye mataifa mengine kwamba bangi inaweza kutumika kama tiba lakini kwa Tanzania bado itaendelea kuwa kwenye orodha ya dawa za kulevya zilizopigwa marufuku.

Aidha, alisema wanaozalisha bidhaa kwa kuweka bangi huwa hawaziweki nembo kwa kuwa ni haramu na kuwahamasisha wananchi kuendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha wahusika wote wanakamatwa na kuchukuliwa hatua.

Waziri Mhagama alisema taarifa ya dunia ya mwaka 2022 inaonyesha kuwa asilimia 40 ya nchi zenye matumizi makubwa zinakumbwa na wagonjwa wa afya ya akili, uhalifu na uvunjivu wa amani.

"Serikali haijakaa kimya, imeendelea na operesheni na kwamba mwaka 2022 tulikamata tani 15.2 za mirungi, kilo 254.7 heroine na kilo 1.7 ya cocaine. Kumekuwapo na mwendelezo wa ukamataji wa dawa ya kulevya aina ya methamphetamine ambapo kwa mara ya kwanza mwaka 2021 zilikamatwa kilo 430.8 na kufuatiwa na gramu 968.7 ambazo zilikamatwa mwaka 2022," alisema.

Pia alisema mwaka 2022 wameshuhudia ukamataji wa dawa nyingine ngeni nchini inayojulikana kama mescaline ambapo gramu 56 zilikamatwa.

"Serikali imefanikiwa kuandaa Mwongozo wa Utoaji Elimu Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini lengo ni kuhakikisha jamii inapata elimu sahihi juu ya tatizo hili.

"Tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya iliendelea kutolewa ambapo kwa mwaka 2022 jumla ya waraibu 871,010 walinufaika na tiba hiyo nchini. Serikali imeendelea kufadhili mafunzo ya stadi za kazi kwa waraibu wanaopata nafuu ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea," alisema.

# Mwinyi asema hawatoficha kitu Ripoti ya CAG Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar (CAG) ya mwaka 2022, itasomwa hadharani Juni 3, mwaka huu, katika viwanja vya Ikulu Zanzibar na kwamba hakuna kitakachofichwa.

Sambamba na hilo, amesema hakuna mtu atakayebaki salama ikiwa atatajwa kwenye ubadhirifu wa mali za umma.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wake wa mwisho wa mwezi Ikulu, Zanzibar jana, alisema ripoti hiyo itasomwa kama ilivyoandikwa na kuwasilishwa wala hakuna kitu kilichobadilishwa.

Dk. Mwinyi alisema hajabadilisha utaratibu wowote wa uwasilishwaji wa ripoti hiyo ambapo mwaka jana alianzisha utaratibu wa kusomwa hadharani kwa sababu kabla ya uongozi wake ilikuwa ikiwasilishwa kimyakimya.

"Mimi ndiye niliyeanzisha utaratibu wa kusomwa kwa ripoti ya CAG hadharani mara nilipoingia madarakani, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kutekeleza dhana ya utawala bora, uwajibikaji na kuwapo kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Sasa wanaosema mbona mwaka huu halijafanyika hilo, acha waone kesho kutwa," alisema.

Dk. Mwinyi alitoa ufafanuzi huo baada ya kuulizwa kwamba tayari amekabidhiwa ripoti ya CAG Ikulu wiki mbili zilizopita lakini hajaisomwa hadharani kama ulivyokuwa utaratibu, jambo ambalo pia limezusha mjadala mkubwa kwa chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo katika mikutano yao ya hadhara.

Alisema miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa kwa atakayebainika kufanya ubadhirifu wa umma ni kushtakiwa kwa kosa la jinai.

Kuhusu watuhumiwa wa wabadhirifu waliotajwa katika ripoti ya CAG ya mwaka 2021, alisema ziko hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa, ikiwamo watendaji wa ngazi za juu serikalini kusimamishwa kazi na kuondolewa katika nafasi zao na kufikishwa mahakamani.

**MIRADI**

Akizungumzia miradi ya maendeleo, alisema serikali anayoiongoza haijavunja sheria ya ununuzi wa miradi iliyoianzisha, ikiwamo ujenzi wa Uwanja wa Amani na ujenzi wa barabara kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume hadi Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Dk. Mwinyi aliwataka wananchi kupuuza maneno ya wapinzani wake kutoka ACT-Wazalendo na kusema kuwa hoja zao zinapaswa kupuuzwa maana hazina ukweli.

"Naona wameanza kupagawa na kasi ya kuleta maendeleo ninayoifanya katika sekta mbalimbali, ikiwamo miundombinu pamoja na ujenzi wa barabara za mjini na vijijini," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kwa sasa wapinzani wameanza kuchanganyikiwa baada ya kuona kasi ya maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ndiyo maana wamejenga hofu kubwa na kuuliza vitu ambavyo havina msingi pamoja na kukosowa katika mambo yasiyostahiki.

"Upuuzi haujibiwi. Wapinzani wameanza kuchanganyikiwa baada ya kuona kasi ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa wameanza kuibuwa hoja ambazo hazina msingi,"alisema.

Pia alitoa ufafanuzi huo baada ya hoja zilizoibuliwa na viongozi wa ACT- Wazalendo katika mikutano ya hadhara kuhusu mikakati ya ubinafsishwaji wa Bandari ya Malindi katika utoaji wa huduma zake, ujenzi wa Uwanja wa Amani na ujenzi wa barabara ambapo walidai haijafuata taratibu ikiwamo za kutangazwa zabuni.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Garagara, Mkoa wa Magharibi Unguja, Mjumbe wa Mkutano Mkuu, Ismail Jussa Labhu, alieleza kushangaa ripoti ya CAG kupelekwa kwa Rais kimpya kimya na baadaye Baraza la Wawakilishi, na kwamba wana hofu kwa kuwa inahusu serikali inayoongozwa na Rais Mwinyi.

**BANDARI**

Alisema kuhusu ujenzi wa Bandari ya Mangapwani ni ujenzi wa bandari kubwa, jumuishi na itahudumia kanda nzima ya Afrika na kukiri kuwa walianza na wawekezaji kutoka Oman, lakini bado fursa ya kuendelea ipo kama wapo tayari kuendelea na haina maana ya kwamba wasizungumze na wawekezaji kutoka nchi zingine.

Alisema lazima serikali ihakikishe mikataba ya ujenzi wa bandari hiyo inamaslahi ya nchi na kuhakikisha bandari hiyo inajengwa kama inavyotaka serikali kwa sababu itakua na sehemu ya mafuta na gesi, kuhifadhia, makontena na eneo huru ambao utakua ni mji wa bandari.

"Wakisema kuwa wawekezaji kutoka Oman kuwa wamejiondoa siyo kweli bado tupo katika mazungumzo lengo ni kupata mkataba ulio bora huo ndiyo ukweli wa mambo na nadhani wanafahamu, lakini wanaposimama katika majukwaa wanafanya makusudi, ili kupotosha umma,"alisema.

Rais Mwinyi akizungumzia hoja ya Bandari ya Malindi alisema haina ufanisi na inaathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa Zanzibar na ufanisi uliokuwapo umesababisha biashara kuwa ngumu Visiwani humo.

"Meli moja inashusha mzigo na kupakia zaidi ya siku sasa hivi sasa tunataka kwa siku mbili tu na ndio maana tumeipa kampuni ya kigeni kuendesha ufanisi wa bandari hiyo kwa mkataba maalum na tunafanya hivyo kwa sababu sisi tumeshindwa," alisema.

Alisema hatua hiyo italeta ufanisi na kuondosha mianya ya upotevu wa fedha kutokana na mambo mengi kufanywa kizamani katika bandari hiyo.


**ARM SOLUTION AUCTION MART AND PROPERTY MANAGEMENT CO LTD**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MuCoBa Bank PLC.** TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA **TAREHE 03-06-2023** NA KUENDELEA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MAGARI MAWILI (2) KAMA YALIVYOORODHESHWA HAPO CHINI.

| NA. | JINA LA MMILIKI | AINA YA GARI NA NAMBA YA GARI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 01 | MUFINDI COMMUNITY LTD | NISSAN PICK-UP<br>T 220 CQU<br>CHASSIS NO. ADNCPUD22Z0037607<br>ENGINE NO. YD25505983T | 03/06/2023 SIKU YA JUMAMOSI KUANZIA SAA TANO ASUBUHI |
| 02 | TRIAS TANZANIA | HILUX PICK UP<br>T 874 AZW<br>CHASSIS NO. AHTFK22G505027156<br>ENGINE NO. ELE107454 | 05/06/2023 SIKU YA JUMATATU KUANZIA SAA TANO ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**

MSHINDI ATATAKIWA KULIPA ASILIMIA **(25%) AU ZAIDI** BAADA YA NYUNDO YA DALALI NA BAKI **(75%)** ITALIPWA NDANI YA **SIKU KUMI NA NNE (14),** TOFAUTI NA HAPO MSHINDI ATAPOTEZA HAKI ZAKE NA MNADA UTARUDIWA UPYA. **MAWASILIANO: 0757 -107 715, 0784 -759 892.**

# Viongozi wa dini: Talaka zisitolewe mahakamani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Mkoa wa Njombe, Shekhe Shabani Dinga, amesema ni vyema suala la talaka kwa wanandoa likaachwa kwa viongozi wa dini husika ili kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani.

Aliyasema hayo katika kikao cha jumuiya hiyo kilichofanyika mjini Makambako, akisisitiza kuwa dini ni muamala unaojitegemea na una taratibu zake nzuri na kila mtu azipe heshima.

"Mahakamani kuna mambo mengi jamani. Mimi ninapata tabu kidogo katika jambo hili. Ndoa inafungwa kanisani, ndoa imefungwa msikitini, ndoa imefungwa kwa sub chiefu, inakwenda kuvunjwa mahakamani. Jamani mwiba ulipoingilia ndipo unapotokea!" Shekhe Dinga alieleza.

Aliongeza: "Ni katiba ya nchi ambayo imeweka utaratibu ndoa iliyofungwa kwa mkuu wa wilaya ndiyo ya mahakamani, mkuu wa wilaya akiona hamweleweki anawasogeza ila sisi ndoa kuipeleka mahakamani sisi viongozi wa dini, wakrito, waislamu, ni kiasi gani tunafeli.

"Mkristo anasema ndoa haivunjiki, kuna masharti yao nao kule wanasema ukifunga ndoa kwa heri. Basi tulete mafunzo ya ndoa, somo si lipo!" Shekhe Dinga alisema ipo haja viongozi wa dini kusimamia masuala ya ndoa ili kupunguza msongamano wa kesi mahakamani.

"Ndoa inasuluhishwa na imani, inajazwa na amani inakuwapo, ni mafanikio ya kiasi gani hayo na yale yanayoshindikana ambayo shetani kayang'ang'ania kabisa, basi tumpelekee mheshimiwa hakimu, ndiyo mfumo wa nchi.

"Lakini mpaka ndoa inafika kwenda kuvunjwa mahakamani ni sisi kuna shida. Sisi viongozi wa dini huku kuna shida kama sio kukosa ushirikiano, waliokaa katika nafasi hizo hawatoshi. Kama sio shinikizo la ufahamu mdogo, lazima viongozi waheshimiwe ili waweze kutusaidia," alieleza.

Askofu wa Kanisa la Yerusalem Mito Mingi, Selenga Nyagawa, alisema viongozi wa dini wana uwezo mkubwa wa kuihubiri amani na kuwatengeneza watu. "Kwa sababu hizo ndoa za kikristo au za kiislamu tunaanzia ndani, kuna mafundisho, ni vyema wakarudi kwetu tuwaelekeze namna ya hiyo ndoa ili waweze kutulia," alisema Nyagawa.

Mwakilishi wa Kanisa la TAG Makambako, Yustina Lenard, alisema wakati umefika kwa viongozi wa dini na kimila kuishi maisha halisi ili kuwaaminisha waumini pindi wanapopata matatizo.

"Ndoa ya mchungaji au ya imamu, shekhe inapokuwa ina shida, mshirika au mtu unayemwongoza kanisani anapokuwa na changamoto hawezi kukufikiria wewe kwa sababu na wewe ya kwako inasumbua.

"Kwa hiyo, mtu anakwenda kwa balozi au mahakamani anaona huko kuko salama na atapata msaada," alifafanua Yustina.

# TANESCO: SGR haitokosa umeme, ratiba kutovurugika

**Na Elizabeth Zaya,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limesema reli ya kisasa (SGR) haitokosa umeme wala kukwama kufanya kazi kwa sababu ya kukatika au kutokea hitilafu katika miundombinu ya umeme.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mhandisi wa Idara ya Mipango ya TANESCO, Lucas Magero, alipozungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya Wiki ya Nishati yanayofanyika Viwanja wa Bunge jijini hapo.

Alisema umeme utakaotumika kuendesha reli ya SGR utakuwa unajitegemea, ukitoka kwenye gridi ya taifa wa kujitosheleza na kwa namna miundombinu yake ilivyowekwa hakutokuwa na uwezekano wa kushindwa kujiendesha au kukwama kutokana na kukatika umeme au hitilafu.

"Umeme utakaotumika kwa ajili ya reli ya SGR utatumia laini yake ambayo haitohusiana na matumizi mengine yoyote na namna laini hiyo ilivyotengenezwa, siyo rahisi kukatika umeme wala kupata hitilafu. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wananchi," alisema Magero.

Aliongeza: "SGR haitokosa umeme baada ya kuanza kwa sababu miradi iliyowekezwa katika uzalishaji wa umeme ni mikubwa sana na tunakwenda kuzalisha zaidi ya kile kinachohitajika.

"Na ikumbukwe kuwa kila baada ya kilomita 50 katika mradi huu wa SGR kutakuwa na kituo cha kupozea umeme chenye uwezo wa kutumia megawati 16. Kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora tuna vituo 11 ambavyo tunakadiria kwamba vitatumia megawati 176.

"Makutupora hadi Tabora tuna vituo vitano vya kupozea umeme, Tabora hadi Isaka vituo vitano, Isaka hadi Mwanza vituo vitano ambavyo makadirio yake ya kutumia umeme ni Megawati 416."

Alisema SGR ikikamilika itatumia umeme wa Megawati 1,000.

Alisema tayari maandalizi ya miundombinu ya umeme katika mradi huo wa reli ya SGR yamefikia asilimia 100 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na kwa Morogoro hadi Makutupora ni asilimia 99.

Kwa upande wa Isaka hadi Mwanza alisema mkandarasi anatarajia kuanza kazi Juni mwaka huu wakati Makutupora hadi Tabora bado wako katika hatua ya upembuzi yakinifu.


TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

## Job Title: Independent Non –Executive Director (1 Position)

Tandahimba Community Bank Plc is a Community Bank established in December, 2005 under the Companies Act, 2002 of the United Republic of Tanzania and started its operations on 10th December, 2008. The Bank is engaged in the business of banking and provision of related services.
The Board of Directors invites applications from suitably qualified candidates who must be a shareholder to fill one position of Independent Non-Executive Director to represent the shareholders of the Bank.

The names of qualified candidates will be submitted to the Annual General Meeting for election.

**Requirements**

1. A professional banker, lawyer, accountant, Insurance or accomplished entrepreneur.
2. Management experience and knowledge in economics, finance, accounting, rural development, agriculture and co operatives.
3. Applicants are required to observe the requirements of Article 108 of the Tandahimba Community Bank Plc Memorandum and Articles of Association and Section 70 of the Banking and Financial Institutions Act which, amongst other things, provide for the qualifications that are required for applicants to possess.
4. The applicant should not be a politician, bankrupt, under 21 years of age.

**NOTE:**

a. *Article 105 of the Bank's MEMARTS states that "The Board of Directors shall have full executive powers and functions of the Company, responsible to the Shareholders' General meeting.*

*The Board of Directors shall have the following duties in addition to those bestowed upon it by the Act.*

*(1) To formulate the policies and strategies as will be recommended by the General Manager*
*(2) To enter into contract with other institutions.*
*(3) To assure that the accounting system is maintained in accordance with acceptance standards and the books of the Company are kept properly, and that the accounts are checked by authorized auditors.*
*(4) To make annual reports on the business in general and future plans of the Company ready for presentation to the Shareholders General meetings.*
*(5) To make regulations as it will be deemed fit for the proper management of the Company.*
*(6) To be appointing authority of the General Manager, Senior Management and the Internal Auditor.*
*(7) To recommend to the Annual General Meeting and external auditor for the Company.*
*(8) Any other duties stipulated under the law.*

b. *Section 70 of the Banking and Financial Institutions Act states that "No member of the management of the Bank who exercises decision making authority with respect to the exercise of any supervisory authority regarding the Bank or financial institutions may hold any office, position or employment in any bank or financial institution while serving as member of management and during the two year period from the date when such a member ceases to be a member of management".*

**Mode of Application**

1. Any Tandahimba Community Bank Plc shareholder who wishes to be elected as an Independent Non-Executive Director must submit an application letter, curriculum vitae, certified copies of relevant academic and professional certificates and awards, two passport size photographs, certified copies of the last page of their passports, National Identity Card (NIDA), letters of recommendation from 3 references and declaration of indebtedness to banks.
2. Notification of receipt of application and other details will be sent to all applicants upon receipt of the applications. Applications must be received by **4.00 p.m. on Friday, 9th June, 2023.** Applicants can also send their applications through **info@tacobabank.co.tz**

**The contact for communication is:**
**The Secretary**
**Tandahimba Community Bank Plc**
**Plot 539 BLOCK C, Namikupa Road**
**P O Box 6, Tandahimba**
**Mtwara.**

**BY ORDER OF THE BOARD**

J. B. Rugambo
**COMPANY SECRETARY**

27th May 2023



TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

*Mwenyekiti na Wanahisa,*

## Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Tisa wa Wanahisa wa Tandahimba Community Bank Plc** utafanyika siku ya Jumamosi tarehe **24 Juni, 2023,** katika **Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU, Tandahimba** kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00)** asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu na Mkutano Mkuu Maalum.**
   - 3.1 Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 18/06/2022
   - 3.2 Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu Maalum uliofanyika tarehe 29/10/2022
4. **Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu na Mkutano Mkuu Maalum.**
   - 4.1 Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 18/06/2022
   - 4.2 Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu Maalum uliofanyika tarehe 29/10/2022
5. **Kujadili na kupokea Taarifa ya Wakurugenzi wenye Dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2022.**
   - 5.1 Taarifa ya Wakurugenzi wenye Dhamana ya Uongozi.
   - 5.2 Taarifa ya Meneja Mkuu.
   - 5.3 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Disemba 2022.
6. **Azimio Maalum la kubadilisha muundo wa sasa wa Tandahimba Community Bank Plc kuwa Benki ya Ushirika.**
7. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi.**
8. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
9. **Kuchagua Mjumbe wa Bodi**
   Uchaguzi wa Mjumbe mmoja (1) wa Bodi atakaewakilisha Wanahisa wa Tandahimba Community Bank Plc.
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano Mkuu ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

**MAELEZO**

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 16/06/2023 na litafunguliwa tena tarehe 19/06/2023.*
2. *Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Makao Makuu ya Benki ya Wananchi Tandahimba tarehe 16/06/2023 na kwenye Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU tarehe 24/06/2023.*
3. *Wanahisa watakaoshindwa kuhudhuria wana haki ya kujaza fomu ya uwakilishi iliyoambatanishwa.*
4. *Wanahisa watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.*

**Kwa mawasiliano tafadhali tumia anuani ifuatayo:**

**Katibu**
**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC,**
**Kiwanja Na. 49- Kitalu 'C', Barabara ya Namikupa,**
**S. L. P. 06, Tandahimba**
**Mtwara.**
**Namba ya Simu: +255 765 405 084**
**Barua pepe: info@tacobabank.co.tz**

KWA IDHINI YA BODI

J. B. Rugambo
**KATIBU**

24 Mei , 2023

# CCM sasa kuja na kadi za kidigitali

**Na Nebart Msokwa,** IRINGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinaandaa kadi za kisasa za kielektroniki za wanachama wake ambazo zitawawezesha wanachama kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Katibu wa Oganizesheni wa CCM, Issa Haji Ussi, maarufu kama Gavu, aliyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Kising'a, Wilaya ya Iringa Vijijini.

Mkutano huo ulikuwa mwendelezo wa ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, katika mkoa huo yenye lengo la kusikiliza kero za wananchi, kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho na kuangalia uhai wa chama.

Gavu alisema kadi hizo za kisasa zitawasaidia wanachama kupata zaidi ya huduma 10 zinazotolewa na taasisi mbalimbali za kiuchumi na kijamii nchini.

Alizitaja baadhi ya huduma ambazo wananchi watakuwa wanazipata kwa kutumia kadi hizo kuwa ni pamoja na bima ya afya, mifuko ya hifadhi za jamii na za kibenki na kwamba zitatumika kadi za kutolea fedha (ATM).

Kadi za awali ambazo zilitengenezwa, alisema zilibainika kuwa na upungufu hasa kutoendana na wakati huu wa maendeleo ya teknolojia, hivyo wakaamua kusitisha kuzitoa ili ziboreshwe kwanza.

"Kadi zetu mpya za kisasa zitaanza kutolewa Agosti, mwaka huu, kwa hiyo nawaomba wanachama wa CCM mwendelee kukiamini chama chenu na kuendelea kuzilipia hizi kadi," alisema Gavu. Katibu Mkuu Chongolo aliwataka viongozi wa chama hicho katika ngazi zote kuendelea kutafuta wanachama wapya ili kuendelea kukiimarisha chama.

Chongolo aliwataka wanachama wa chama hicho kutojibu mashambulizi pale wanapotukanwa na vyama vya upinzani na badala yake wao waitumie miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali kuwajibu.

Alisema serikali imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maendeleo hasa katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara pamoja na sekta ya kilimo na hivyo akaeleza kuwa miradi hiyo inatosha kuwajibu wapinzani wanaoikosoa serikali.

Kwa mujibu wa Chongolo, lengo la chama hicho ni kuendelea kushika dola, hivyo lazima kifanye kazi ya kuwaletea wananchi maendeleo ili waendelee kukiamini na kukichagua kwenye chaguzi mbalimbali.

"Kuna baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani wao kazi yao ni kutukana matusi, sasa sisi hatuwajibu kwa matusi na badala yake tunawajibu kwa kutekeleza miradi ya maendeleo, wakitukana waonyeshe shule, waonyeshe vituo vya afya na barabara," alisema Chongolo.

Mbunge wa Isimani, William Lukuvi, alisema katika hilo, wananchi wamekuwa wakikabiliwa na uhaba wa maji kwa muda mrefu lakini kwa sasa tatizo limepungua kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Alisema kwa sasa asilimia kubwa ya wananchi wanapata maji ya bomba na kwamba maeneo machache yaliyobakia wanaendelea na utekelezaji wa miradi itakayomaliza kabisa tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji mkoani humo ni nzuri kwa maelezo kuwa maeneo ya mjini upatikanaji wa huduma hiyo ni asilimia 84 na vijijini ni asilimia 74.



Ofisa Elimu Wilaya ya Kinondoni, Mtundi Nyamhanga (wa tatu kulia), akikabidhi cheti cha mwanafunzi bora kwa wanawake wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Feza, Sophia Kileo, wakati wa mahafali jijini Dar es Salaam juzi. Wa nne kulia ni Mwenyekiti wa shule za Feza, Ismail Yilmaz. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Awamu ya pili DMDP kudhibiti mafuriko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTEKELEZAJI wa Mradi Uendelezaji Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP) awamu ya pili utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 800 unatarajiwa kuanza hivi karibuni, huku asilimia 74 ya fedha zikielekezwa kwenye miundombinu kudhibiti kero zinazokabili ikiwamo mafuriko.

Kutokana na hatua hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema ofisi yake itahakikisha utekelezaji huo unakuwa na mafanikio makubwa na kuonya dosari zilizojitokeza kwenye awamu iliyopita zisijirudie.

Akizungumza jana jijini hapo baada ya kushuhudia utiaji saini mikataba kati ya ofisi hiyo na makandarasi watakaosanifu mradi huo, Kairuki alisema mahitaji ya fedha kwa ajili ya miundombinu ya mkoa huo ni Sh. trilioni 1.8 na serikali kupitia Wizara ya Fedha itaendelea kupambana ili kubuni miradi mingine.

Kairuki alisema mradi huo utatatua kero mbalimbali zikiwamo ujenzi wa makazi holela, miundombinu duni ya usafiri, mabadiliko ya tabianchi kwa mkoa wa Dar es Salaam zinazosababisha mafuriko na utupaji taka ngumu ovyo.

"Wabunge wa maeneo husika hakikisheni mnasimamia halmashauri zenu ili utekelezaji wa mradi huu uwe na mafanikio na kusiwapo dosari, TAMISEMI tutakuwa makini kuhakikisha kwamba mradi huu awamu ya pili unatekelelezwa kwa mafanikio makubwa, tunaamini tutakuwa tumejifunza kupitia utekelezaji wa awamu ya kwanza," alisema.

Aidha, aliwataka makandarasi hao, Mhandisi Consultancy Ltd & Luphan (Halmashauri za Temeke na Kigamboni), Nimeta Consultancy Ltd (Kinondoni na Ubungo) na UWP Consultancy Ltd (Jiji la Dar es Salaam) kuzingatia masharti ya mikataba yao.

"Mjue kuwa kusaini mkataba ni jambo moja, utekelezaji ni jambo lingine hivyo zingatieni mikataba mliyosaini maana hatutarajii muwe kikwazo, ikitokea tutarudi kwenye mkataba kuangalia masharti yaliyowekwa," alisema Kairuki.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema mradi huo ulikuwa kilio kikubwa kwa wabunge wa mkoa wa Dar es Salaam ambao kila bajeti walikuwa wakisimama kuhoji.

Awali, akitoa maelezo ya mradi huo, Mratibu wa Miradi ya Serikali kupitia mikopo ya Benki ya Dunia, TAMISEMI na TARURA, Mhandisi Humphrey Kanyenye, alisema Benki ya Dunia imeridhia mkopo wa kutekeleza mradi huo mwezi Machi mwaka huu.

Alisema mkoa huo unakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo usafiri, utunzaji taka ngumu, mafuriko na miundombinu isiyokidhi kiwango hivyo mradi huo unaenda kuziondoa.

Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile, alisema wabunge watakuwa wakali katika kusimamia mradi huo na kutaka viporo vya DMDP awamu ya kwanza vikamilike.

# ACT-Wazalendo yalia na umaskini Rukwa

**Na Julieth Mkireri,** SUMBAWANGA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuongeza bajeti katika kilimo na kuwekeza kujenga viwanda ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na wakulima.

Akizungumza na wakazi wa Sumbawanga mkoani Rukwa jana, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Doroth Semu alisema Mkoa wa Rukwa pamoja na kuongoza katika uzalishaji wa mazao, bado umeendelea kutajwa kama mkoa maskini.

Doroth alisema serikali inatakiwa kuongeza bajeti katika kilimo kwa kuwa mazao yanayozalishwa na wakulima wanayauza kama bidhaa ghafi na hivyo kuendelea kuishi maisha duni.

"Kwa hiyo, tunataka serikali iwekeze katika viwanda vidogo ndani ya mikoa ya Rukwa na Katavi ili mazao yachakatwe na yawe na thamani na kwa hatua hii itamkomboa mwananchi," alisema.

Aliongeza kuwa chama hicho kwa sasa kinataka serikali kuboresha mifumo ya kilimo kwa kuwekeza katika viwanda ili mazao yanayozalishwa katika mkoa huo yawe na tija kwa wakulima.

Alisema mkoa huo hususani wilayani Sumbawanga, wapo wananchi wanaohudumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na hawajapewa fedha tangu mwaka huu uanze, hivyo ni jukumu la serikali kuwapa fedha wanazostahili za kuanzia Januari mwaka huu.

Alisema chama hicho katika kukabiliana na vikwazo hivyo, kimejipanga kuanzisha sera ya hifadhi ya jamii ambayo mwananchi atapata bima ya afya, atawekeza na atapata bima ya afya.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema Mkoa wa Rukwa unatajwa kuwa na kiwango cha juu cha umaskini wa mahitaji muhimu na chakula licha ya wananchi hao kuwa na ardhi na wanazalisha lakini wanachozalisha wanakiuza kwa bei ya chini.

Alisema chama hicho pia kinataka wabadhirifu wote wakiwamo wa Mkoa wa Rukwa waliotajwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), wafikishwe katika vyombo vya sheria.

# Chongolo ataka usimamizi ujenzi skimu ya umwagiliaji

**Na Nebrt Msokwa,** IRINGA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameiagiza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kusimamia vizuri ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Mkombozi iliyoko katika kata ya Mboliboli Wilaya ya Iringa ili ikamilike kwa wakati.

Skimu hiyo inajengwa na serikali kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 55 na inatarajiwa kutumika kwenye mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 15,000 katika eneo hilo ambalo wananchi wanazalisha mpunga.

Chongolo alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kukagua skimu hiyo kwa lengo la kuangalia maendeleo yake ambapo aliipongeza serikali kwa kuamua kujenga skimu hiyo.

Alisema mradi huo unatakiwa kukamilika ndani ya miezi 18 kama ambavyo mikataba ya makandarasi wanaotekeleza imeainishwa, ili wananchi waanze uzalishaji mapema na kuongeza tija katika kilimo.

"Naipongeza sana serikali kwa kuanzisha mradi huu lakini ili tija yake ionekane tume ya taifa ya umwagiliaji inatakiwa kusimamia vizuri, sisi huko serikalini tutaweka msukumo ili fedha za kuwalipa makandarasi zije kwa wakati," alisema Chongolo.

Aliwataka wananchi watakaokuwa wanaitumia skimu hiyo kuhakikisha wanaitunza miundombinu, ili itumike kwa muda mrefu na tija yake iendane na fedha ambazo serikali imewekeza katika eneo hilo.

Ofisa Umwagiliaji wa Wilaya ya Iringa, Mhandisi Julius Lazaro, alisema skimu hiyo ilianzishwa na wananchi ambao walikuwa wanaitengeneza kwa kutumia mbinu za kienyeji na hivyo tija yake ilikuwa ndogo kwa sababu walikuwa wanazuia maji na mchanga.

Alisema wananchi hao walikuwa wanalima ekari 5,000 pekee kwa mwaka mzima, lakini watakapokamilisha ujenzi wa skimu hiyo watakuwa wanalima zaidi ya ekari 15,000 ambazo zipo kwenye bonde hilo.

Alisema uzalishaji wa sasa ni tani 6,000 za mpunga lakini skimu hiyo itakapoanza kutumika uzalishaji utaongezeka mara sita na kufikia tani 36,000 na hivyo kuwainua wananchi wa eneo hilo kukua kiuchumi.

"Mkataba wa ujenzi wa skimu hii ni wa miezi 18 na ikikamilika itawasaidia wakulima kulima mara mbili kwa mwaka tofauti na sasa ambapo wanalima mara moja pekee," alisema Mhandisi Lazaro.

Diwani wa Mboliboli, Yusuph Samba, aliishukuru serikali kwa kuwasaidia kuboresha skimu hiyo kwa maelezo kuwa walikuwa wanapata shida kwa muda mrefu na kulikuwa kunaibuka migogoro mingi.


## UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TANESCO

## TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED
## GENERAL PROCUREMENT NOTICE

**Name of Borrower/Recipient's Country: UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**Name of Project: KAKONO HYDROPOWER PROJECT**

## GENERAL PROCUREMENT NOTICE

1. The Government of the United Republic of Tanzania has received a loan from the African Development Bank (the "Bank") and French Development Agency; and a grant from European Union Delegation to finance the Kakono Hydropower Project, herein referred to as the "Project."

2. The principal objective of the Project is "to increase on-grid energy production from least-cost renewables to address the electricity deficits in north-western Tanzania."

3. The Project includes the following main components: -

   A. Construction of Kakono hydropower plant estimated at 87.8 MW,
   B. Construction of power evacuation facilities,
   C. Project administration and management,
   D. Implementation of the Environmental and Social Management and Monitoring Plan.

4. The procurement of goods, works and services, financed by the Bank, will be carried out in accordance with the Bank's "Procurement Policy for Bank Group Funded Operations" dated October 2015 in line with the provisions stated in the loan agreement. The Specific Procurement Notice in relation to the "Consultancy services for construction supervision and management of the 87.8 MW Kakono Hydropower Project in Kagera Region" was published on 24th April, 2023. Other Specific Procurement Notices are expected to be available on February, 2024.

5. Interested bidders may obtain further information, and should confirm their interest, by contacting: -

**Tanzania Electric Supply Company Limited**
**Secretary Tender Board**
**Umeme Park Building, Morogoro Road, Ubungo Area,**
**P. O. Box 9024**
**Dar es Salaam**

**Email: sec.tenderboard@tanesco.co.tz ; pmuprojects@tanesco.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mpango wa mafunzo JKT unapaswa kuungwa mkono

**HIVI** karibuni, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) lilitangaza kuwa limeandaa mazingira ya kuwezesha vijana wote wanaomaliza kidato cha sita mwaka huu, kujiunga na mafunzo ya kijeshi kupitia taasisi hiyo. Lengo la mafunzo hayo, kama ilivyo kwenye malengo la kuanzishwa kwake, ni kuwajenga vijana wa Kitanzania katika hali ya ukakamavu na uzalendo kwa nchi yao.

Tangu kuanza kwa jeshi hilo mwaka 1963, Watanzania wengi, wakiwamo wale wanaomaliza kidato cha sita na vyuo mbalimbali, walijiunga na jeshi hilo kwa mafunzo ya kijeshi kwa mujibu wa sheria. Mafunzo hayo yalianza kufanyika kwa miezi sita baadaye mwaka mmoja kabla ya kufutwa mwaka 1994 kutokana na sababu mbalimbali lakini yalirejeshwa miaka ya karibuni na kufanyika kwa miezi mitatu.

Viongozi mbalimbali wakiwamo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mawaziri wakuu wa wakati huo, Edward Sokoine, Rashidi Kawawa na aliyekuwa Spika wa Bunge la Tanzania, Chifu Adam Sapi Mkwawa, walijiunga na mafunzo hayo. Hiyo yote ilikuwa kuonyesha kuwa mafunzo hayo ni muhimu na kila Mtanzania hasa vijana wanaomaliza masomo kidato cha sita na vyuo wanajiunga.

Licha ya kufundishwa ukakamavu na hali ya kujiamini, Watanzania hao pia walifundishwa namna ya kujitambua katika kukabiliana na mazingira yanayowazunguka pamoja na kushiriki masuala ya kijamii na kujitegemea kimaisha.

Wakati wa mafunzo hayo, wale waliokuwa wamepitia mafunzo ya fani mbalimbali kama tiba, kilimo, mifugo na ufundi, walipelekwa katika vitengo mbalimbali vinavyohusiana na fani zao. Waliokuwa wamemaliza kidato cha sita, walifanya kazi katika bustani, mashamba na mifugo na huko walipata maarifa ya namna mbalimbali za kufanya kazi kwa kujituma na kwa weledi.

Hata wale waliokuwa wametoka katika familia za watu mashuhuri na mambo yote yanafanywa na wafanyakazi wa ndani nyumbani kwao, walibadilika na kuwa wachapakazi wazuri, yote ikiwa ni kuwajenga kujitegemea katika majukumu mbalimbali watakapoingia katika ajira na maisha kwa ujumla.

Kimsingi, mafunzo hayo yalikuwa kama daraja la kuwafunza vijana namna ya kukabiliana na changamoto za kimaisha na wengi wao waliyamudu ndiyo maana waliokuwa wamepitia JKT, walipoingia katika kazi na kupewa majukumu mbalimbali, walionyesha uwezo mkubwa na kuleta tija kwenye taasisi walizofanya kazi.


Mpango huo wa JKT kuwataka vijana wote waliomaliza kidato cha sita na taaluma mbalimbali za ngazi ya cheti na diploma kujiunga na mafunzo hayo, umekuja wakati mwafaka kutokana na mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa yamechagizwa na mmomonyoko wa maadili.

Ni imani kwamba vijana hawa watakapojiunga na mafunzo hayo, bila kujali muda watakaotumia, watabadilika na kuwa watu wenye uzalendo na wenye kujitambua na kujiamini tofauti na ilivyo sasa katika makundi mbalimbali kutokana na kutojishughulisha na kazi mbalimbali za kujiingizia kipato. Matokeo yake vijana hao wamekuwa watu wa kukaa vijiweni na kutegemea vitu vya bure, jambo ambalo ni rahisi kuingia katika mitego ya kurubuniwa na kujihusisha na mambo maovu.

Ni ushahidi ulio wazi kwamba vijana wengi, hasa wa kiume, hivi sasa wameelekeza fikra katika michezo ya kamali, maarufu kama kubeti, badala ya kukijita kazi uzalishaji na kazi mbalimbali ambazo zitawaondoa katika utegemezi na lindi la umaskini.

Mpango wa JKT kuwachukua vijana wote waliomaliza elimu ya sekondari ya kidato cha sita na vyuo, unapaswa kuungwa mkono na wazazi, walezi na wananchi kwa ujumla kwa kuwa una nia njema kwa taifa katika kurejesha uwezo wa vijana kujitambua na kutumia maarifa yao kwa maendeleo yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Pwani inang'aa miradi yote kukubaliwa na Mwenge

**HIVI** karibuni, Mwenge wa Uhuru ulihitimisha mbio zake mkoani Pwani, ukiwa umepitia miradi 99 yenye thamani ya Shilingi trilioni 4.46 huku kukiwa hakuna hata mradi mmoja uliokataliwa.

Mkuu wa Mkoa huo, Alhaji Abubakari Kunenge, alitoa taarifa hiyo wakati akikabidhi Mwenge kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ambaye alisema mkoani kwake, Mwenge ulitarajiwa kutembelea miradi 32 yenye thamani ya Shilingi bilioni 23.4.

Ingawa inawezekana ipo mikoa ambayo Mwenge huo umepita na kukubali miradi yote ya maeneo hayo, lakini kwa mkoa wa Pwani ambao nimefanikiwa kusikia taarifa, unaweza kuwa ni wa kutolea mfano.

Kwa nini? Kwa sababu imekuwa ni kama jambo la kawaida kuona kila mwaka Mwenge ukikataa baadhi ya miradi inayotekelezwa chini ya kiwango kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo rushwa.

Labda nikumbushie kidogo kwa miaka iliyopita nikianzisha mbio za Mwenge huo za mwaka 2021 ambapo miradi 49 ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 65.3, ilikataliwa baada ya kutiliwa shaka kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo ujenzi chini ya kiwango na kukosekana ukweli wa thamani halisi ya pesa.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, katika kilele cha mbio hizo kilichofanyika Chato mkoani Geita mwaka huo. Katika taarifa yake, akafafanua kuwa miradi hiyo ni kwenye wilaya 38 katika ya wilaya 150 zilizotembelewa na mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huo wa 2021.

Ukija katika hitimisho la mbio hizo mwaka jana mkoani Kagera, ilitolewa taarifa kuwa miradi 65 ya thamani ya Shilingi bilioni 12 ilikataliwa baada ya kugubikwa na dosari ikiwamo, rushwa, uzembe na ubadhirifu.

Taarifa iliotolewa mbele Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ilionyesha miradi 1,263 yenye thamani ya Shilingi bilioni 650 ilipitiwa na Mwenge huo mwaka jana.

Kwa mazingira hayo, ni wazi kuna haja ya kujifunza jambo kutoka katika mkoa wa Pwani ili kuepuka kutumia vibaya fedha za walipa kodi na kukwamisha maendeleo ya nchi yao.

Lakini pia ninadhani ipo haja ya kuwachukulia hatua za kisheria wanaohujumu miradi ya maendeleo, kwani bila kufanya hivyo, inawezekana maendeleo ya nchi yakazidi kusuasua.

Itakumbukwa Rais Samia Suluhu Hassan, aliwahi kutoa maelekezo kwa Taasisi ya Kupambana na Kudhibiti Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa Zanzibar ( ZAECA) kufanya uchunguzi na kuchukua hatua stahiki kwa wote waliobainika kufanya ubadhirifu wa fedha za umma kwenye miradi 65 iliyokataliwa na Mwenge.

Rais pia alielekeza kila kiongozi kusimamia matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuhakikisha inafanyika kuzingatia ubora kulingana na thamani ya fedha.

Lakini akawataka Watanzania kuyaenzi mema yaliyoachwa na hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ikiwamo kukataa rushwa, uzembe na ubadhirifu wa fedha za umma.

Aidha, Rais aliwapongeza viongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa uaminifu na uzalendo walioonyesha, ikiwa ni pamoja na kuikataa miradi yenye mashaka na dosari mbalimbali.

Mwaka jana, Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa kwa siku 195 kwenye halmashauri 195 na kuweka mawe ya msingi na kuzindua miradi 1,263 yenye thamani ya Shilingi bilioni 650.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la kituo hicho la kulaani matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi za taifa na mapori tengefu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# LHRC yalaani ukiukwaji wa haki za binadamu maeneo ya hifadhi

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimelaani matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu dhidi ya wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi za taifa na mapori tengefu, kikipendekeza hatua nne za kumaliza vitendo hivyo.

Akitoa tamko la kulaani matukio hayo mbele ya waandishi wa habari katika makao makuu ya kituo hicho Kijitonyama, Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alitaja hatua za kuchukuliwa ni pamoja na serikali kuhakikisha watuhumiwa wa vitendo hivyo wanakamatwa na kufikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

"Tunapendekeza pia askari wa hifadhi za taifa na misitu kuzingatia misingi ya haki za binadamu wakati wa utekelezaji wa amri za kuwaondoa na kuwahamisha wananchi wanaovamia maeneo hayo kinyume cha sheria," alisema.

Dk. Anna pia alitaja hatua ya tatu ya kuchukuliwa ni wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi kuacha kuvamia maeneo yaliyoainishwa kama hifadhi au mapori tengefu kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi huyo pia alisema kituo kinaishauri serikali kuunda tume maalum au kikosi kazi ambacho kitafanya kazi ya uhakiki wa mipaka katika maeneo yote ya hifadhi na mapori tengefu.

"Tunashauri hivyo kwani kwa muda mrefu yamekuwa yakisababisha migogoro kati ya wananchi na askari wa mamlaka za wanyamapori," alisema.

Dk. Anna alisema kituo hicho kinasikitishwa na taarifa za matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanayofanywa na askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kwa jamii ya watu inayoishi karibu na hifadhi ya taifa na mapori tengefu.

"Matukio haya yamekuwa yakijumuisha kupigwa, vitendo vya mauaji, kudhalilishwa, kufukuzwa katika maeneo yao na kunyang'anywa mifugo kinyume cha sheria," alisema.

Alifafanua kuwa baada ya kutolewa kwa taarifa za vitendo hivyo katika vyombo vya habari, kituo hicho kilifanya utafiti wa kina ili kubaini ukweli wa taarifa hizo.

"Kwa mfano, utafiti wetu katika eneo la Mbarali ulibaini kuwa taarifa hizo ni za kweli kwani zilithibitishwa na mamlaka za serikali za wilaya akiwamo mkuu wa wilaya na katibu tawala," alisema.

Alifafanua kuwa mbali na uongozi wa wilaya, hata Waziri wa Maliasili na Utalii alithibitisha maelezo kwamba wizara ilitoa Sh. milioni moja kwa waathirika wote waliojeruhiwa kutokana na vitendo vya ukatili kama mkono wa pole.

Alisema matukio ya migogoro baina ya mamlaka ya hifadhi na wananchi yamekuwa chanzo kikubwa cha uvunjifu wa haki za binadamu kwa kipindi kirefu.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo migogoro hiyo imekuwa ikijitokeza kuwa ni Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Pori Tengefu la Wilaya ya Geita mkoani Geita na Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA).

"Tunaomba ifahamike kwamba LHRC kama taasisi ya haki za binadamu, hatuungi mkono wala hatuna nia ya kuunga mkono wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi yaliyoainishwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania," alisema.

Alifafanua kuwa kituo hicho kinazitaka mamlaka zinazohusika na uhifadhi zikiwamo TANAPA, TAWA na TFS, kuzingatia misingi ya haki za binadamu wakati utekelezaji wa amri za kuwaondoa na kuwahamisha wananchi katika maeneo ya hifadhi.

# Umeme wa Bwawa la Nyerere kuingia gridi ya taifa karibuni

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema megawati 2,115 zitakazozalishwa katika Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP), zinazotarajiwa kuanza kuingia hivi karibuni kwenye gridi ya taifa, zitatosheleza matumizi ya nishati nyumbani kwa nchi nzima.

Aidha, shirika hilo limesema limefanya tathmini na kubaini kuwa kuna miundombinu chakavu katika eneo la usambazaji, hivyo linahitaji Sh. trilioni 4.42 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza na wahariri kuhusu miradi inayotekelezwa na shirika hilo na mpango mkakati wa kumaliza kabisa upungufu wa umeme nchini.

Alisema kwa sasa shirika lina wateja milioni nne wa nyumbani na kwamba kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kila nyumba ina wastani wa watu watano, hivyo kwa sasa matumizi ya umeme majumbani ni asilimia 50 ya matumizi ya jumla ya umeme nchini, huku wateja wa viwandani wakiwa 4,000 ambao nao wanatumia asilimia 50 iliyobaki.

Mkurugenzi hiyo alisema mipango ya shirika hilo ni kufikia uzalishaji wa megawati 5,000 kufikia mwaka 2025 na kwamba limeweka mipango ya hadi mwaka 2035 kwa miradi ya umeme ya uzalishaji na usafirishaji watakayoitekeleza katika kipindi hicho. Alisema kuanza uzalishaji kwa bwawa la JNHPP kutasababisha umeme wa uhakika lakini hawatapunguza bei kwani wanataka kujizatiti kiuchumi, ili kuendelea kutekeleza miradi mingine ya kimkakati ya nishati hiyo.

"Hatutatoa mapendekezo ya kushusha bei kwa mamlaka inayodhibiti nishati kwa sababu tunataka tujiimarishe zaidi kiuchumi, ili tupate uwezo wa kuwaunganishia umeme Watanzania wengi zaidi ambao hawana nishati hii.

Na hivi karibuni tulifanya tathmini ambayo imebaini tuna miundombinu chakavu katika eneo la usambazaji hivyo tunahitaji trilioni 4.42 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu hiyo kwa hiyo utaona hapa kwamba tunahitaji fedha zaidi," alisema.

Chande alisema Bunge lililopita lilipitisha Sh. bilioni 500 kwa kazi hiyo na kwamba Rais alishapitisha fedha hizo na tayari wameshaanza kufanya manunuzi na makandarasi wako kazini akiongeza kuwa kwa awamu ya kwanza wameanza na trilioni 1.9 ambako kuna miradi 29 ya usambazaji ambayo itasaidia kutatua mambo ya umeme kukatika.

Alisema kwa sasa wanatathmini kuhusu hali ya upatikanaji wa umeme kwa ajili ya kukuza uchumi na kwamba wamebaini kuwa katika kila watu 1,000,000 zinahitajika megawati 1,000 hivyo kwa Tanzania yenye watu milioni 60 inahitaji megawati 60,000.

"Kwa sasa tuna megawati 1,800, mwaka jana tulikuwa na megawati 1,600 na Mwalimu Nyerere ikiingia tunatarajia kufika 3,800. Afrika Kusini mnakosikia kelele za mgawo wanazalisha megawati 54,000 kwa hiyo bado tunahitaji kuzalisha umeme mwingi zaidi," alisema.

Alisema pamoja na Afrika Kusini kuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 54,000, megawati 32,000 pekee ndizo zinaingia kwenye gridi ya taifa kutokana na miundombinu yao kusafirisha umeme kutokuwa katika hali nzuri.

"Sisi tunaendelea kuzalisha umeme kwa wingi kwa sababu mahitaji ya umeme yanazidi kuongezeka kwa kasi kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar na Tanzania Bara, Misri inazalisha zaidi ya megawati 40,000, Uturuki megawati 80,000 na Dubai 70 na sisi tutaendelea ili tufike huko," alisema.

Alisema kwenye awamu ya kwanza walitengeneza mkakati wa miezi 18 mpaka 24 kwa sasa wako kwenye awamu ya pili ya 'Tanesco Tuko Kazini' ambapo wanatekeleza mambo yote waliyopanga kwenye awamu ya kwanza.

Chande alisema mkakati huo ulikuwa na vipaumbele huku akibainisha kuwa baada ya mwaka mmoja wamefanya tathmini na kubaini kuwa matokeo yamekuwa mazuri sana kwani wamefikia wateja wengi.

"Kipaumbele chetu cha kwanza kilikuwa wateja kwasababu wateja wetu ndio wanatufanya tuje kazini kwa hiyo tulijitahidi kuweka watu ambao watawahakikishia huduma bora wateja wetu, kipaumbele kingine kilikuwa ni ufanisi, miradi ya kimkakati, kutafuta rasilimali na kusimamia vihatarishi na mwisho namna ya kutoa taarifa kwa wateja na ukifanya tathmini tumefanikiwa sana," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Warioba ashauri mabadiliko sera, miongozo kuinua kilimo

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MKUU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Jaji mstaafu, Joseph Warioba, amesema mpango wa mageuzi ya kilimo utafanikiwa endapo serikali itabadilisha sera na miongozo ya kilimo ambayo itawafanya vijana kupenda kushiriki shughuli za kilimo.

Akizungumza juzi katika kilele cha maadhimisho ya Kumbukizi ya 18 ya Hayati Edward Moringe Sokoine, yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, (SUA) mjini Morogoro, alisema iwapo yatafanyika mabadiliko hayo kutakuwa na mafanikio.

"Ajira ni tatizo kubwa kwa vijana, lazima tujenge utamaduni wa vijana kupenda kilimo, kwani pasipo kukipenda kilimo ni vigumu kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo," alisema Warioba.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema serikali imejipanga kuhakikisha vijana wanashiriki katika kilimo chenye tija kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wengine kupitia mpango wa mageuzi ya kilimo na kukuza uchumi.

"Kwa sasa kuna mpango wa mageuzi ya kilimo, serikali imejipanga kisawasawa kuhakikisha kuwa vijana wanashiriki katika kilimo chenye tija kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri katika sekta hiyo muhimu," alisema Nguli.

Pia alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, takwimu zinaonyesha kuwa kundi kubwa la Watanzania ni vijana ambao ni asilimia 34.5.

Kutokana na takwimu hizo, alisema serikali imeweka mikakati kuhakikisha kuwa vijana wanashiriki katika shughuli za uchumi kwa kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wenzao katika sekta mbalimbali.

"Ninawapongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kuja na kauli mbiu nzuri ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema 'mazingira wezeshi kwa vijana kushiriki katika kilimo Tanzania, sera, miongozo na utendaji, ni kaulimbiu muafaka kwa kuwa ndicho hasa serikali inachokifanya kwa kuwezesha kundi la vijana kuzalisha mazao ya kilimo na mnyororo wa thamani, sambamba na shughuli nyingine za uzalishaji," alisema.

Waziri wa Kilimo mstaafu, Paul Kimiti, alisema vijana wanapaswa kushirikiana katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili.

"Hatufanani kwa maumbile wala uwezo wa kufikiri kama vilivyo vidole, lakini kila mmoja ana umuhimu mkubwa katika kutimiza lengo ambalo ni kuleta maendeleo ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla, hivyo vijana mnapaswa kushirikiana bila kujali tofauti zenu ili kwa pamoja muweze kujikwamua kutoka kwenye changamoto zinazowakabili," alisema Kimiti.

Awali, Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema chuo hicho kitaendelea kujikita katika kufanya tafiti mbalimbali za kilimo kwa lengo la kuhakikisha kuwa kilimo kinazidi kukua kwa kuwa na mbinu bora za kisayansi zitakazochagiza uzalishaji wa tija.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tempo Africa, Pendo Lema (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa 'application' maalumu kwa ajili ya simu za mkononi na tovuti inayohusiana na taarifa za utalii. Kushoto ni Meneja Biashara wa kampuni hiyo, Thadei Swai na Meneja Uhusiano, Millian Lema. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC apokewa kwa mabango madai waziri kupora ardhi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Rebecca Nsemwa, amejikuta amepokewa kwa mabango na vilio kutoka kwa wananchi wa vijiji vya Dalla na Mbwade, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, wakishinikiza kurudishiwa zaidi ya ekari 1,000 zinazodaiwa kuchukuliwa bila utaratibu na aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina.

Wananchi hao waliokusanya katika kijiji cha Dalla walisimamisha msafara wa mkuu huyo wa wilaya na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama, ukiwa njiani kwenda kwenye mkutano na wananchi wa vijiji vya Dalla, Kongwa na Mbwade kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakabili.

Wakiwa na mabango yaliyobeba ujumbe mbalimbali ukiwamo kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kusikia kilio chao, walisema wamedhulumiwa ardhi na Mbunge huyo wa Kisesa (CCM) ambaye katika serikali ya awamu ya tano alikuwa waziri.

Akiwasilisha kero kwa mkuu huyo wa wilaya, Consolata Mchuma alisema kwa zaidi ya miaka minane, wananchi wali teseka kutokana na kuchukuliwa kwa ardhi yao.

Baada ya kutangaziwa na serikali ya kijiji kupatikana kwa mwekezaji Mpina, alisema wananchi walikubali kumpa ekari 300 huku akitakiwa pia kujenga madarasa manne yakiwamo mawili Shule ya Msingi Dalla na mawili Shule ya Msingi Kilengezi na kuendelea kulima lakini mpaka sasa hajatekeleza makubaliano hayo.

Alisema mwaka 2016 (Mahuma) akiwa mjumbe wa serikali ya kijiji hicho, Mpina aliwasilisha barua ya kutaka kuongezewa eneo lingine la ekari 700 lakini wanakijiji walikataa huku wakimtaka afike ofisini ili atekeleze ahadi yake lakini aliendelea kukaidi.

Kwa mujibu wa Mahuma baadaye alitwaa hilo eneo kwa madai kwamba amelinunua jambo ambalo hajahusisha kwenye mkutano wa kijiji wala kuidhinishiwa na muhtasari wa kuridhiwa na wanakijiji.

Naye Diwani Mstaafu wa Viti Maalum Tarafa ya Mvuha, Marrystella Chamlungo, akizungumza huku akibubujikwa na machozi, alisema pamoja na Mpina kuchukua eneo hilo, alipitisha greda kwenye mazao yao na kuwasababishia hasara na alipoitwa kwa ajili ya kulipa fidia aligoma kutekeleza.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbwade, Salumu Malozo, alisema mwekezaji Mpina, amemega eneo katika vijiji vitatu vya Mbwade, Kongwa na Dalla na kusababisha kuwapo kwa mgogoro wa wananchi wa vijiji hivyo.

Diwani wa Mvuha, Mfaume Amani, alisema wakati anaingia madarakani mwaka 2015 alikuta mgogoro huo ulionza mwaka 2009 na suala hilo lilifikia kwenye vikao mbalimbali kikiwamo cha halmashauri kwa ajili ya kurudishwa kwa eneo hilo kwa kuwa taratibu hazikufuatwa.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Halima Mtawazo, alisema mwekezaji huyo alizungumza na halmashauri ya kijiji yenye wajumbe 25 na kwamba maombi yake hayakukamilika kwa kuwa wajumbe hao hawakuitisha mkutano wa kijiji ili kufanya uamuzi wa kuidhinisha au kukataa. Kwa mantiki hiyo, alisema hakukamilisha taratibu zinazotakiwa.

Baada ya kusikiliza hoja kuhusiana na mgogoro huo, Nsemwa aliagiza kuundwa kwa timu ya wataalamu itakayopitia nyaraka za pande zote pamoja na kupima eneo la shamba hilo ili kubaini ukubwa wake pamoja na kuainisha mipaka.

Mkuu huyo wa wilaya alisema lengo la timu hiyo ambayo itafanya kazi kwa siku 14 ni kubaini uhalali wa nyaraka na upimaji wa mipaka ili kila upande upate haki yake kwenye vijiji hivyo.

Alimtaka Mpina kutoa ushirikiano kwa timu hiyo ili kumaliza mgogoro na kuwawezesha wananchi kuendelea kushiriki katika shughuli za kilimo kwenye eneo hilo.

# ACT-Wazalendo yaingilia kati wakulima kutolipwa bil. 6/-

**Na Julieth Mkireri,** PERAMIHO

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe ameishauri serikali kuwasaidia wakulima 1,008 ambao hawajalipwa fedha zao tangu 2020 baada ya mahindi yao yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni sita kukusanywa na mfanyabiashara ambaye hajalipa hadi sasa.

Wakulima hao wanadai kukusanya mahindi yao kwa mfanyabiashara aliyefahamika kwa jina la Christopher Njako. Baada ya kuchukua mahindi hayo aliahidi kulipa kwa wakati, lakini hadi sasa utekelezaji haujafanyika.

Zitto aliyasema hayo juzi katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na chama hicho katika Viwanja vya Tamasha mjini Peramiho mkoani Ruvuma.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, mfanyabiashara huyo alikamatwa na baadaye kuachiwa na hadi sasa hajawalipa wakulima hao.

"Kauli yetu serikali ihakikishe wakulima wanalipwa fedha zao kuondoa sintofahamu iliyopo kwa sasa kutokana na kutopata haki yao baada ya mahindi yao kuchukuliwa na mfabyabiashara huyo," alisema.

Wakulima hao wa mahindi kutoka mikoa mbalimbali katika Soko la Mkako wilayani Mbinga wanadaiwa kukusanya magunia ya mahindi 84,302.

Inadaiwa kuwa baada ya ukimya, waliandika barua ya malalamiko mwaka 2020 kwa Naibu Waziri wa Kilimo wakieleza madai yao na kuiomba wizara kuwasaidia kupata fedha zao. Ofisi ya Naibu Waziri wa Kilimo ilijibu barua hiyo Desemba 18, 2020 ikikiri kupokea barua kutoka kwa umoja wa wakulima wa mahindi na kuahidi kufanyia kazi suala hilo.


Mwaka 2021 baada ya ukimya kuendelea kutanda wakulima hao waliandika barua nyingine kwa Rais wakifikisha malalamiko yao baada ya mfanyabiashara huyo kutowalipa fedha zao tangu alipochukua mahindi yao.

Waziri Kivuli wa Biashara wa ACT Wazalendo, Halima Nabalang'anya, aliitaka serikali kuwa ma mkakati imara wa uwekezaji wa viwanda hususani eneo la mahindi, ili kuliongezea thamani zao hilo.

Alisema kwa sasa zipo mashine za kukoboa na kusaga pekee. Viwanda vikijengwa mkoani Ruvuma unaoongoza kwa uzalishaji wa mahindi, vitasaidia kutoa ajira kwa vijana. Alisema Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko pia inatakiwa kununua mazao kwa faida ili kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa wakulima.

Mratibu wa Jimbo la Madaba, Hussen Kaliango, alisema kuwa na madiwani na wabunge wa vyama vya upinzani ni moja ya njia ya kuleta maendeleo katika maeneo husika.

Kaliango pia aliwatoa hofu wananchi ambao wanadai kutishiwa wakiingia katika vyama vya upinzani wanaohudumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wataondolewa. Alisema huo ni upotoshaji.



## RITA yagusa wengi elimu ya mirathi, wosia

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) imeendelea kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa sambamba na elimu kuhusiana na kuandika na kuhifadhi wosia wilayani Babati.

Tukio hilo lilifanyika wakati wa kampeni iitwayo Mama Samia Suluhu Hassan iliyozinduliwa Mei 24, mwaka huu mkoani Manyara kwenye viwanja vya stendi ya zamani.

RITA imeweka kambi zaidi ya siku 10 mkoani Manyara, kufanya usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa huku ikiendela kuelimisha jamii kuondokana na dhana potofu iliyotawala miongoni mwa jamii kubwa kuwa wosia ni uchuro.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa tukio hilo, Msajili kutoka RITA, Bestina George alisema kuwa idadi kubwa ya wananchi wamejitokeza kwa wingi kupata elimu kuhusu mirathi na wosia huku wengi wakiamini wosia ni uchuro.

"Wananchi wamejitokeza kusajili vyeti japo wengi sana wamekua wakitaka kufahamu kuhusu mirathi maana inaonekana familia nyingi zina migogoro katika eneo hilo,"alisema Bestina.

Aidha, wananchi waliipongeza RITA kwa kutoa vyeti ndani ya siku moja na elimu kuhusu usimamizi wa mirathi kuandika na kuhifadhi wosia ambayo wao binafsi walikua wanaamini kuandika wosia n kujichuria.

RITA Inaendelea kutoa Huduma ya usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa mkoani Manyara hadi Juni 2, mwaka huu katika viwanya vya stendi ya zamani wilayani Babati kwenye kampeni iitwayo Mama Samia Legal Aid.

# TAKUKURU yabaini upungufu miradi ya bilioni 10/-

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MIRADI 18 ya maendeleo ya Sh. bilioni 10 iliyochunguzwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Tanga imebainika kuwa na upungufu ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za manunuzi, kasi ndogo ya utekelezaji na ubora hafifu.

Aidha katika moja ya miradi hiyo kwenye Wilaya ya Korogwe, TAKUKURU imebaini madiwani wake waliingilia mchakato wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwenye Sh. milioni 173.

Jana, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Mariam Mayaya, alisema miradi hiyo ni kati ya miradi ya maendeleo 70, ya zaidi ya Sh. bilioni 41 iliyochunguzwa.

Alisema pia wamebaini vikundi vimeshindwa kutunza taarifa za fedha na vingine kugawana fedha za mikopo hiyo badala ya kuifanyia kazi waliyoombea.

Kutokana na mapungufu hayo, TAKUKURU imeeleza kuwa tayari wamechukua hatua kwa kufungua jalada la uchunguzi.

Pia katika mradi wa ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni mbili TAKUKURU imebaini baadhi ya vifaa vya ujenzi vilinunuliwa kwa bei kubwa kuliko uhalisia na baadhi ya vifaa vya ujenzi vilinunuliwa idadi kubwa kuliko mahitaji.

Alisema katika ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe iliyotengewa Sh. milioni 150, wamebaini mradi hauendelei baada ya kusitishwa kwa mkataba wa ujenzi kati ya fundi na halmashauri jambo ambalo limekwamisha uendelezaji wa mradi.

Kuhusu ujenzi wa Mradi wa Maji Chekelei (Korogwe) wa Sh. bilioni mbili ambao ulikuwa na tatizo la kifedha alisema Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), imeshafanya maombi ya fedha ya kukamilisha mradi huo Wizara ya Maji.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (kulia), alipotembelea banda la benki hiyo wakati wa mkutano mkuu wa 37 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) jijini Arusha juzi. NBC ni mmoja wa wadhamini wa mkutano huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ofisa Elimu aitaka jamii kuvunja ukimya kuhusu hedhi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

OFISA Elimu wa Shule za Msingi wa Jiji la Arusha, Hussein Bakari, amesema iko haja kwa jamii kujitokeza na kuvunja ukimya kuhusu hedhi salama kuanzia ngazi ya familia ili kuwasaidia watoto wa kike hasa wenye ulemavu kufahamu mapema namna ya kujisitiri.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi wenye ulemavu, wazazi, walezi na walimu wanaofundisha shule za msingi zenye vitengo maalum katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Mwakilishi kutoka taasisi ya Little Angel Foundation (LAF), Rephrin Kombe, alisema kwa kushirikiana na wadau wengine wametoa elimu kwa wazazi, walezi wenye watoto walemavu na walimu wa vitengo maalum kutoka shule zilizopo jijini humo.

Alitaja shule hizo hizo ni Themi, Arusha School, Meru, Makumbusho, Baraa, Kaloleni na Uhuru.

Mmoja wanafunzi walionufaika, Linda Salvatory, alisema sodo hizo zitawasadia hasa wale ambao wanatoka kwenye familia duni na kuomba wazazi na walezi wenye watoto hao kuwasaidia wanapokuwa kwenye hedhi

Mratibu wa Mradi wa Afya ya Uzazi na Hedhi Salama wa Shirika la Fida FPCT, Seth Johnson, alisema kupitia mradi huo, unaotekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini wanasaidia kuondoa mila na desturi zinazokwamisha mazingira ya hedhi salama kwa wanafunzi.

# Mpango asifu benki kuchochea maendeleo ya serikali za mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango ameipongeza Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa ushirikiano mkubwa inayouonyesha kwa mamlaka za serikali za mitaa nchini kuchochea ukuaji wa maendeleo hususani katika ngazi ya msingi.

Dk. Mpango pia ameonyesha kuridhishwa na kasi ya ukuaji wa benki hiyo kiasi cha kulipa gawio kwa serikali lenye thamani ya Sh. bilioni sita kutokana na mafanikio makubwa ya kibiashara iliyoyapata mwaka 2022. Akizungumza jana na uongozi wa Benki ya NBC alipotembela banda la benki hiyo katika Mkutano Mkuu wa 37 Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) unaoendelea jijini Arusha.

Dk. Mpango alisema ushirikiano mkubwa wa benki hiyo na mamlaka za serikali za mitaa nchini kupitia utoaji huduma za kifedha na uwezeshaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo umekuwa chachukatika ukuaji wa maendeleo katika ngazi ya msingi.


Aliitaka menejimenti ya benki hiyo kuendeleza jitihada hizo ili mchango wake kwa wananchi uwe na tija zaidi sambamba na kuchangia zaidi pato la serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Elibariki Masuke, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Binafsi wa Benki ya NBC, alionyesha kuridhishwa na uhusiano mzuri kati ya benki hiyo na ALAT huku akiahidi kuendelea kushirikiana na jumuiya hiyo katika jitihada zake za kukuza utawala bora na maendeleo nchini. Pia alionyesha matumaini kuhusu uwezekano wa ushirikiano zaidi kati ya taasisi hizo mbili.

Masuke alisema benki hiyo pia ni miongoni mwa walipakodi wakubwa waliochangia zaidi ya Sh. bilioni 66.5 katika Hazina ya taifa mwaka kwa 2022.

"Katika kipindi hicho hicho, benki ililipa gawio la serikali lenye thamani ya bilioni sita. Tuna furaha kuwa mshirika muhimu na mshiriki katika ajenda ya maendeleo ya kitaifa na tunahakikisha kuendelea kusaidia. Milango yetu inaendelea kuwa wazi ili kutumikia si tu serikali na watumishi wa umma, bali watanzania wote kwa ujumla," alisema.

Benki ya NBC ni miongoni mwa wadhamini wa mkutano huo ambao ulifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais.





# Aliyekutwa na nyara za serikali aachiwa huru

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tabora imemwachia huru mshtakiwa, Embe Ramadhani mkazi wa Kabanga Kata ya Chabutwa wilayani Sikonge mkoani Tabora aliyeshtakiwa kwa kosa la kukutwa na nyara za serikali.

Ramadhani alikutwa na vipande 16 vya mnyama aina ya palaha pamoja na kilo mbili za nyama pori vya Sh. milioni 588.9.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, John Mdoe, alisema mshtakiwa huyo alikutwa na nyara hizo pasipokuwa na kibali chochote kutoka kwa wahusika.

Katika shauri hilo upande wa Jamhuri uliwasilisha na mashahidi watano pamoja na vielelezo vitano ambavyo ni hati ya ukamataji mali, maelezo ya onyo ya mshtakiwa na fomu ya kuharibu mali ya serikali.

Awali katika utetezi wake mshtakiwa alikana kukutwa na nyara hizo baada ya kukamatwa na kupelekwa katika ofisi za maliasili, huku mke wake aitwaye Rehema alisema wakati anakamatwa hapakuwapo na kiongozi yeyote ambaye alishuhudia, hivyo kutilia mashaka ushahidi uliotolewa na Jamhuri.

Katika ushahidi uliotolewa na Jamhuri inadaiwa kwamba Elnesti Charles ambaye maelezo yake yapo chini ya kifungu cha Sheria cha 34 B, Kifungu Kidogo cha Pili C cha Sheria ya Ushahidi, maelezo ya Jamhuri kutoka kwa Matei Joane alimtaja shahidi ambae alikuwapo wakati wa ukamataji alikosea kutaja jina badala ya Ernest alisema Evalist, hivyo kufanya maelezo hayo ya shahidi ambaye hakufika katika Mahakama hiyo kuwa na upungufu.

Mdoe alieleza kuwa kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 34 katika kipengele kidogo 'e' juu ya mazingira ya ukamataji kinasema maelezo kama hayo kabla hayajapokelewa na Mahakama ni lazima shahidi yeyote apewe taarifa siku 10 kabla ya ushahidi huo kupelekwa mahakamani.

Hakimu Mdoe alisema kwamba katika shauri hilo kulikuwa hakuna mtiririko mzuri wa nyara zilizokamatwa na kupelekwa sehemu siyo stahiki kama ilivyoelekeza serikali, hivyo mnyororo huo wa kesi hiyo ulikatika, kwamba mshtakiwa hawezi kutiwa hatiani na Mahakama.



Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga (wa pili kushoto), akimsikiliza Msanifu Majengo kutoka Sotta Mining, Elmon Mafwenga (kulia), akielezea mfano wa nyumba 10 za kisasa watakazojengewa wananchi wa Kata ya Igalula, ambao makazi yao yapo ndani ya eneo la mradi ikiwa ni sehemu ya mchakato wa kuwahamisha ili kupisha mradi wa Mgodi wa Dhahabu wa Nyanzaga, wakati wa maonyesho ya nyumba hizo chini ya mpango wa RAP katika kijiji cha Nyabila wilayani humo mkoani Mwanza. Kushoto ni Mratibu wa Uhamishaji Makazi kupisha mradi, Mhandisi Paul Gongo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mtoto ashambuliwa na fisi akichota maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MTOTO Joyce Sengerema (10) mkazi wa kijiji cha Kiloleli, Kishapu mkoani Shinyanga, amenusurika kifo baada ya kushambuliwa sehemu mbalimbali za mwili na fisi wakati akichota maji katika Mto Manonga.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Kishiwa Maganga, akisimulia tukio hilo baada ya kumfikisha mtoto huyo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Shinyanga, alisema tukio hilo lilitokea Mei 27, mwaka huu, majira ya saa 12:00 alfajiri.

Alisema mtoto huyo aling'atwa kichwani, shingoni na ubavuni na kwamba kilichonusuru ni kuwapo kwa mwananchi mmoja aliyekuwa akilima kando ya mto huo na kusikia kelele, hivyo kufika na kumkimbiza fisi huyo na kufanikiwa kumwokoa.

"Mtoto wangu huwa ana tabia ya kuamka kila siku alfariji kwenda kuchota maji katika Mto Manonga, lakini hiyo juzi nilishangaa kusikia kuwa ameshambuliwa na fisi. Namshukuru Mungu aliokolewa na asingekuwapo mtu jirani, sasa hivi tungekuwa tunazungumza mengine," alisema Maganga.

Daktari aliyekuwa zamu, Jesse Samweli, alisema mtoto huyo alifikishwa hospitalini akiwa katika hali mbaya baada ya kushambuliwa na fisi huyo na kubainisha kuwa bado wanaendelea kumpatia matibabu.

Diwani wa Kiloleli, Edward Manyama, aliwaomba maofisa wanyamapori wilayani Kishapu kuwasaka fisi wote ambao wanazurura ovyo ili kuzuia tatizo hilo la kushambulia wananchi hasa wanawake na watoto ambao huamka alfajiri kwenda kutafuta maji.

# Waiangukia serikali kunusuru uuzwaji kituo yatima

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya Waislamu wa Msikiti wa Ijumaa uliopo mkoani Mwanza wameiomba serikali pamoja na jamii kusaidia kunusuru uuzwaji wa kituo cha Yatima Islamic Foundation.

Kituo hicho kinapigwa mnada kwa amri ya Mahakama kutokana na kudaiwa Sh. milioni 109 na aliyekuwa msimamizi wa kituo hicho.

Kituo hicho kinatarajiwa kuuzwa baada ya aliyekuwa msimamizi wake kushinda kesi mahakamani na kulipwa Sh.milioni 78 kama sehemu ya stahiki zake pamoja na Sh.milioni 31 kama gharama alizotumia kuendesha kesi hiyo ya madai ya malimbikizo ya mshahara.

Wakizungumza na waandishi wa habari mmoja wa waumini hao, Masood Hamis alisema baada ya Sherally Hussein ambaye alikuwa msimamizi wa kituo hicho kushinda kesi ya madai hukumu yake inatarajiwa kukaziwa Juni 7, mwaka huu.

Alisema hukumu hiyo inaonyesha ameshinda, kwamba kituo hicho kinatakiwa kuuzwa, kwamba waliiomba jamii kusaidia msikiti huo kulipa deni hilo ili kuwasaidia watoto yatima wanaoishi katika kituo hicho.

"Ikiwa atashinda kesi huko Mahakama Kuu basi sisi waislamu wa Msikiti wa Ijumaa tunaomba jamii kuunganisha nguvu kulipia fidia hiyo ili kituo kiendelee kuwalea yatima na kudhibiti ongezeko la watoto wa mitaani," alisema Masood.

Aidha aliongeza kuwa kwa watu wote wenye nia njema juu ya kituo hicho wajitokeze kutoa chochote husuani pale itakapohitajika kumlipa Sherally ili watoto waendelee kupatiwa huduma zote ikiwa ni pamoja na elimu, malazi na malezi.

Naye Ramadhani Ally ambaye ni mhumini katika msikiti huo alisema kituo hicho kinahudumia watoto wengi yatima, hivyo kuiomba serikali kutizama kwa makini namna ya kuwasaidia ili kukinusuru ili kiendelee kubaki katika mikono ya dini hiyo.

Inadaiwa kuwa Sherally Hussein alikishtaki kituo hicho katika Mahakama ya Kazi akihitaji kulipwa stahiki zake za muda mrefu baada ya bodi ya wadhamini wa kituo hicho kumwondoa katika nafasi yake kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kutokuridhishwa na utendaji wake.




Ukurasa 12

**BERNARD MEMBE:**

**Mwanasiasa aliyegombea vyama viwili tofauti uchaguzi ukifuatana**




Tanzania yakumbushwa kubeba diplomasia ya sayansi na ubunifu



Ukurasa 14

**BOLA TINUBU**

**Kiongozi aliyechaguliwa kwa kura kiduchu zaidi tangu mwaka 1999**


# siasa

JUMATANO MEI 31, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


MCHWA FEDHA ZA UMMA

# Dawa uwepo sheria kutenga maslahi binafsi, kazi za umma

**Na Dk. Felician B. Kilahama**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inaonyesha utafunaji wa fedha za serikali ambao chanzo au chimbuko linahusishwa na kutozingatia maslahi ya taifa kwa baadhi ya watunga sera na wafanya maamuzi.

Badala ya kujali Tanzania yenye neema wanawekeza kwenye maslahi binafsi hata utekelezaji wa miradi au shughuli za umma kuwa na ufanisi duni.

Mazoea hayo huleta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ambao ndiyo walengwa wakuu. Katika makala iliyotangulia ilimalizika kwa mfano wa kukarabati ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kutumia fedha kidogo alizopata kutoka serikali kuu lakini hakuwa tayari kufafanua zaidi.

Hata hivyo, baada ya kupitia wilaya na halmashauri kadhaa kilichogundulika ni kwamba fedha zinatolewa lakini matumizi yake, kwa kiasi kikubwa, yalikuwa hayaendani na malengo ya kile kilichokusudiwa au kupangwa.

Kimsingi, hali kama hiyo matokeo yake ni kushuhudia 'madudu' mengi kama zilivyobainishwa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU).

Hali ilivyo suala la kuzuia rushwa nchini bado halijawa shwari ndiyo maana katika harakati za kupambana na kutoa na kupokea mlungula ubadhirifu wa fedha za umma unajitokeza mara-kwa mara.

Kichocheo kwa hayo yote, kinatokana na 'uhuru au ruksa' waliyonayo viongozi wakuu wa serikali kushiriki masuala ya biashara na kunufaika wao na jamaa zao.

Tunaweza kusema hiki ni kikundi cha watu wachache walioshikilia usukani serikalini na



Huduma za kijamii kama madaraja yanajengwa chini ya kiwango kutokana na ubadhirifu.
**PICHA: MTANDAO**

hapohapo wanayo maslahi binafsi kupitia milango mbalimbali ya kibiashara.

Inakuwepo dira au maono ya kitaifa yanayotakiwa kutekelezwa na serikali kuu na serikali za mitaa na katika michakato ya kuweka mipango kutekeleza malengo, ndipo 'kujipenda' zaidi kwa baadhi ya wahusika serikalini kunapoanzia.

Fedha zipo, mipango ya kuzitumia kutekeleza malengo yanayokusudiwa ipo changamoto inakuja, 'mimi mhusika nitanufaika vipi'?

Kwakuwa wahusika wanazo nguvu za kisera na uwezo wa kufanya maamuzi papo kwa hapo wanao 'uhuru fulani' unawampa mwanya kuhusika na maslahi binafsi hivyo wanajitahidi kadri wawezavyo kupindisha mambo kwa faida binafsi.

Kuna usemi fedha ni sabuni ya roho, tutajiuliza kivipi? Sina jibu wakati huo kwamba nyakati hizi ibilisi amejikita katika fedha hivyo kugeuza akili za wengi.

Hivyo, kuwa na madaraka serikali yanapochanganyika na roho za kupenda fedha sana' kuliko maslahi ya taifa dira au maono na mipango ya kitaifa pamoja na utekelezaji wake vinabaki zaidi kwenye makabrasha na au nadharia kuliko kivitendo.

**KUDHARUA UMMA**

Maono binafsi yanapewa kipaumbele zaidi kuliko ya kitaifa. Kwa msingi huo viongozi wengi na watendaji serikalini wapo lakini hawabebi moja-kwa-moja dira auaono ya taifa kama timu moja badala yake mwelekeo na kutii haja binafsi unadhoofisha taifa. Katika mazingira kama hayo, kwa vyovyote vile, fedha zilizolenga kukidhi malengo ya kitaifa 'zitaelekezwa yalipo maslahi binafsi'.

Kumbuka usemi 'hazina ya mtu ilipo ndiko na roho yake ilipo' hivyo, yaliyo katika nafsi ya mhusika, ndiyo yanayopewa kipaumbele zaidi kuliko mengineyo.

Aidha, hali hiyo inaashiria ukosefu wa uzalendo kwa baadhi ya Watanzania na kusababisha kukosekana umoja imara kitaifa hivyo kuzorotesha utekelezaji maono, mipango ya kitaifa. Ndiko kuwapo watendaji kuvutia kwao na kuchukua chao mapema.

**UMOJA KITAIFA**

Dhana ya kujenga umoja wa kitaifa ulio imara siyo tu katika demokrasia na siasa pekee bali pia katika utendaji, serikali kuu na zile za mitaa.

Wakati huohuo, viongozi warejee kwenye misingi ya utawala imara kwa kuzingatia kanuni muhimu ikiwa ni pamoja na kutenganisha shughuli za kibiashara na watendaji serikalini.

Kanuni aliyokuwa nayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere irejeshwe. Siyo dhambi kukiri kwamba kuna kukosea sasa ni kujirekebisha itakuwa jambo la kheri kuliko shari.

Kwa mataifa yaliyoendelea kama Marekani au barani la Ulaya, suala la biashara kwa watendaji serikalini ni kitu cha kawaida kutokana na wahusika kutenganisha maslahi binafsi na shughuli za umma.

Lakini kwa mataifa yanayoinukia kiuchumi ni majanga matupu kama ripoti za CAG na TAKUKURU zinavyobainisha kila mwaka.

Zinahitajika juhudi kubwa kujenga timu za kitaifa na watendaji wazalendo, watumishi wenye uchungu na nchi yetu na wenye maslahi kwa taifa na Watanzania wote, mijini na vijijini.

Dhana hii maana yake ni uwepo wa timu za kitaifa zenye dira na maono mapana kwa taifa yaliyoandikwa kwenye nafsi na mioyoni mwao. Kuanzia mkubwa aliye juu kimadaraka, hadi mtendaji wa chini akiwa ni mhudumu ofisini, kwa mnyororo wote, lao liwe moja kuhakikisha vya taifa vinatekelezwa bila kuchechemea na mafanikio yaonekane kama ilivyokusudiwa.

Vilevile, kuwepo na mikakati thabiti ya kuzuia au kugundua ubadhirifu na kuepusha matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma, mapema na si kungojea mwaka uishe ni hasara kubwa.

Mazoea ni kuona ripoti za CAG au kuiagiza TAKUKURU kufanya uchunguzi wakati mambo yameishaharibika. Ndani ya wizara, taasisi za serikali, mashirika na mawakala wake.

Idara ya wakaguzi wa ndani iongezewe nguvu ili iweze kufuatilia kwa ukaribu kinachofanyika wakati wa michakato ya manunuzi au matumizi mengine ya fedha za umma.

Kadhalika, kungekuwepo na jicho la ndani kunusa harufu ya rushwa au ubadhirifu na kuarifu mamlaka mapema kabla malipo au wizi haujatekelezwa.


**INAENDELEA UK. 12**

BERNARD MEMBE: 1953 - 2023

# Mwanasiasa aliyegombea vyama viwili tofauti uchaguzi ukifuatana

**Na Ani Jozeni**



KIFO cha Bernard Membe (69), aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa miaka mingi, kimewastua Watanzania wengi kwani haikuwahi kusikika kuwa anaugua au amelazwa wakati akiwa kiongozi na hata alipoondoka madarakani.

Ila halikuwa jambo la ajabu kwani wapo viongozi wa kisiasa na wasomi wanaofahamika vyema walioondoka duniani wakiwa vijana hata zaidi, iwe ni kwa ajali au ni maradhi yaliyowashambulia ghafla. Ni vihatarishi vya kibinadamu ambavyo kimsingi havizuiliki, na ndiyo mustakabali mzima wa masuala ya imani.

Maisha ya Membe katika siasa hayakuwa na 'mikiki wala makeke,' wengi wakimwona kama mpendwa au kipenzi cha mfumo wa siasa wakati wa awamu ya nne, kama wanadiplomasia watangulizi kama awamu au enzi za Ali Hassan Mwinyi na Baba wa Taifa Julius Nyerere.

Mwalimu Nyerere alitaka nafasi yake itwaliwe na mwanadiplomasia Salim Ahmed Salim, lakini akakwamishwa na Kamati ya CCM, hata hivyo akafaulu awamu iliyofuata, akawezesha kuchaguliwa kwa Benjamin Mkapa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje mwenye kuheshimika.

Aliyekuwa mwanadiplomasia nguli wa awamu ya tatu na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Jakaya Kikwete, akawa ndiye mteule wa CCM, naye akataka iwe vivyo hivyo kwa Membe.

Licha ya kuwa viongozi wakuu wa nchi siyo lazima watoke miongoni mwa wanaoongoza Wizara ya Mambo ya Nje, kuna jambo ambalo wanadiplomasia wanaongeza katika uongozi, yaani umuhimu wa kusikiliza na kujali kila sauti inayoongea. Katika diplomasia kila siku unatafutwa muafaka, maelewano yenye tija kwa kiasi fulani kinachokubalika kwa pande zinahusika. Mwanadiplomasia lazima awe mvumilivu, msikivu na pia mnyenyekevu, anayeepusha shari hata wakitofautiana.

Wanaomfahamu kwa karibu wanasema hizo ndizo zilikuwa sifa za hayati Membe, na kwa maana hiyo rais wa awamu ya nne unaweza kusema aliitakia mema nchi kuwa na kiongozi msikivu kama yeye alivyokuwa, kwamba hataingia katika kishawishi cha udikteta wala kuwaburuza Watanzania.

> Licha ya kugombea 2015 akiwa nafasi yatano bora, alishindwa na nafasi ya mgombea uchaguzi kupewa JPM, hata hivyo mwaka 2020 aligombea kupitia ACT – Wazalendo.

Hata Mwalimu Julius Nyerere alikiri mara kwa mara kuwa mfumo wa katiba unamruhusu rais kuwa dikteta akitaka, hivyo kuwa msikivu na mpole au kutoonea watu ni tunu ya mtu binafsi katika mfumo huo, kuwa si kukosa madaraka ila kutoyatumia vibaya. Ulazima wa madaraka hayo ni suala jingine, na unaweza kusema hata wanaotaka kuyaondoa wanajua umuhimu wake.

Kimsingi mwanadiplomasia huyo aliona kuna nafasi ya yeye kuwa kiongozi mkuu wa nchi, na kwa vile ilikuwa dhahiri anaungwa mkono katika ngazi za juu sana, yeye mwenyewe na watu wake wa karibu wangeamini hilo linatosha kumpa nafasi hiyo ya kuongoza taifa.

Tatizo ni kuwa kutangaza nia hakutokei hivi hivi ila katika mazingira mahsusi ya kisiasa, ambako wafuasi wa vyama huangaliana wao kwa wao kujua nani anaweza kukubalika kikamilifu zaidi.

Kwa kuinuliwa ndani ya CCM kama mgombea mtarajiwa halafu ACT-Wazalendo, kukubalika kwa Membe kulidhihirika kama ilivyokuwa kwa hayati Augustine Mrema au Edward Lowassa, ila mazingira ya kampeni yake mwaka 2020 yalikuwa ya kushtukiza na yalishangaza pia.

Uwepo wa Membe katika uwanja wa siasa, kama ilivyo hivi sasa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ni kielelezo kimojawapo cha uwazi wa mfumo wa sasa wa siasa, na kuwa kama una mtaji wa kukubalika unaweza kugombea popote. Ila tofauti na wapinzani wa mfumo huo wanavyosema, nguvu zote haziko tu katika mikono ya rais kwani naye pia anategemea uongozi wa pamoja, kwa kujali wananchi wanataka nini.

Ndiyo maana baadhi ya wadau wa siasa walioandika kitabu hivi karibuni 'I am the State, Whispered a President from Chato', ikitafsiriwa kama 'Rais aliyenong'ona Mimi Ndiye Dola kutoka Chato' hawakuliona hilo. Alitumia nguvu ya umma, watu wakawa nyuma yake, alipoanza kutumbia majipu lakini tofauti zinaonyesha kuwa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali leo zinaonyesha kuwa majipu yamerudi.

Kama ambavyo wachambuzi tofauti wamemtaja, Membe alipata ubunge katika eneo lake la kuzaliwa la Mtama hasa kutokana na kukubalika serikalini, hakuwahi kutajwa kuwa na sifa ya mtu aliyevuna mapesa huku na kule kwa njia yoyote ile, iwe ni biashara au miradi serikalini.

Kwa vile alikuwa waziri kwa muda mrefu miaka tisa haielekei kuwa alikuwa na uhaba wa fedha, ila hakuwahi kuwa na sifa ya utajiri kama wenzie kadhaa.

Ambacho hatuwezi kujua, na hasa baada ya kuondoka waziri huyo wa siku nyingi, ni tofauti ambayo ingekuwepo endapo Membe angepita kama mgombea wa CCM, ukiuliza swali hilo ni wazi utavuna makundi mawili ya majibu, na hapa hakuna cha upinzani na CCM ila kuchukulia poa na mabadilikoo ya kina. Wanaomfahamu Membe, na hasa ukaribu wake na uongozi wa awamu ya nne, wangetazamia kiongozi mpole, mwanademokrasia ambaye Baba wa Taifa angesema 'wala rushwa hawatamwogopa.' Ndiyo hapo kuna kujikanganya katika lugha rasmi hasa miongoni mwa makundi huria yasiyo ya kiserikali na mtazamo wa kina miongoni mwa jamii.

Mtawala anayependwa na makundi ya kiraia na sehemu kubwa ya watawala serikalini ni yule asiyeogopwa na walarushwa, ila wananchi wanamtaka huyo ambaye watamwogopa, ajikusanyie madaraka ayatumie kuwanyoosha watawala, alete maendeleo.

**KUGOMBEA MARA 2**

Ina maana kuwa Membe aligombea mara mbili na vipindi vyote viwili vikifuatana ila wakati haukuwa wake, kwani mwaka 2015 hisia za kisiasa zilikuwa za kuhitajika mabadiliko na siyo mwendelezo wa moja wa moja wa awamu ya nne, aliokuwa akisimamia Membe.

Licha ya kugombea 2015 akiwa nafasi yatano bora, alishindwa na nafasi ya mgombea uchaguzi kupewa JPM, hata hivyo mwaka 2020 aligombea kupitia ACT -Wazalendo.

Inaelekea kufikia mwaka 2020 kwanza hakuwa na msingi au mtaji wa kutosha kumyumbisha JPM na kwa hali yoyote ile mabadiliko ambayo punde yalitazamiwa kuja ilikuwa ni mabadliko ya dira ya uchumi na ushirikiano na nchi nyingine kukuza uchumi, siyo kurudi tulipokuwa mwaka 2015

Buriani Komredi Membe, ulisimamia taswira iliyofifia, pengine ya kutobadilika kisera maana watu walitaka mabadaliko huenda ingekuwa ni kuendeleza furaha iliyokuwepo mwaka 2015 ambayo ni uwazi wa serikali , uelewano bungeni, uhuru wa kutoa maoni na kukosoa. Hakuna majibu rahisi kwa hilo iwapo angekuwa Rais Bora wa Tanzania, ila cha muhimu ni Membe alikuwa kiongozi mwenye utulivu, mwenye kupenda uelewano na mwanadiplomasia wa kimataifa.

## Dawa uwepo sheria kutenga maslahi binafsi, kazi za umma

**INATOKA UK. 11**

Hivyo, kufanya mamlaka kuchukua hatua haraka mambo yasitetereke na wahusika kufikishwa mbele ya sheria au uongozi ipasavyo.

**MASHIRIKA YA UMMA**

Kuna mashirika kulingana na ripoti ya CAG yanapata hasara.

Sawa matarajio ni kutengeneza faida lakini kabla ya kukimbilia kuyafuta, uchunguzi wa kina ufanyike kujiridhisha kiini cha kupata hasara kijulikane bayana ili makosa kama hayo yasirudiwe.

Itakapogundulika kuwa kumekuwepo uzembe na ubadhirifu au wizi ama udanganyifu katika utekelezaji wa majukumu hatua zichukuliwe kwa waliohusika na kusababisha hasara.

Watakaobainika kuhusika na hasara au wizi ama rushwa hatua kali za kisheria zichukuliwe pamoja na kuwafilisi ili kilichopotea kirejeshwe.

Sheria ziwe kali sana ili kusiwepo mianya ya mahakama kuwaonea huruma ili mradi-mhusika avune alichokipanda.

Kama ni wema kwa watanzania atavuna mema, lakini ukiwa ubadhirifu avune adhabu kali vilevile, kuwepo umakini katika harakati za kuyafuta mashirika yaliyobeba alama za kitaifa.


Watendaji wanaosababisha hasara kwa uzembe wajione kuwa wanajiweka kitanzi wenyewe na wasionewe haya wala huruma. Ukitaka kumuanganiza nyani usimwangalie usoni atajifanya analialia umwonee huruma wakati ni mharibifu.

Ni aibu kubwa kwa baadhi kushindwa kusimamia shughuli za kitaifa kikamilifu na kwa weledi na kwa maslahi ya taifa .

Ripoti za CAG na TAKUKURU, ifike mahali ziwe ni za kupongeza zaidi kuliko hali ilivyo sasa. Hakuna lisilowezekana taifa, serikali na Watanzania wachukue hatua stahiki kurekebisha uovu kwa faida ya wote.

# Tanzania yakumbushwa kubeba diplomasia ya sayansi na ubunifu

**Na Sabato Kasika**




Leonard Ndimubansi, mtetezi wa diplomasia ya sayansi na teknolojia. **PICHA: SABATO KASIKA**

MIONGONI mwa manufaa mengi ili nchi iendelee ni elimu ya sayansi, teknolojia, ubunifu na utafiti. Vyote vikipatikana kupitia utafiti, kufundishwa shuleni, vyuo vya kati na vikuu.

Kwa ujumla ni mambo yanayofanikisha maendeleo na kuifanikisha Tanzania kuendana na dunia ya sasa, likiwa ni suala muhimu.

Ndivyo Leonard Ndimubansi, anavyoanza kuelekeza katika mazungumzo na Nipashe, akitamani kushikwa mkono aonane na Rais Samia Suluhu Hassan, amweleze jinsi ambavyo Tanzania inaweza kuwa na diplomasia ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Anataka kuwe na diplomasia inayofanya kazi ya elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuwezesha taifa kuwa na wataalamu wa kuunda vitu mbalimbali zikiwamo ndege na vifaa vya kielektroniki badala ya kuvinunua nje.

"Mimi ni mwanaharakati wa kutumia elimu, sayansi, teknolojia na ubunifu (ESTU), ninaamini kuwa ili kuharakisha kukuza uchumi, suala la diplomasia hiyo haliepukiki,"anasema Ndimubansi.

Anataka uwekezaji mkubwa kwenye maeneo hayo matatu anayoamini kuwa taifa litakuwa na wataalamu na wasomi, lakini litajenga viwanda vya kutosha, kutengeneza bidhaa kutokana na rasilimali zilizoko nchini kama madini, gesi, misitu, mazao ya kilimo.

"Badala ya mabalozi wetu kutafuta wawekezaji kuja nchini kuvuna rasilimali zetu na sisi kubaki madalali wa , wauzaji, masoko na watumiaji wa bidhaa za nje, mabalozi wetu badala yake watafute masoko ya bidhaa zetu za viwandani, kama ndege, vito vya madini, dawa badala ya kuviagiza toka nje. Hii itaipaisha uchumi wa Tanzania haraka hata kuwa kama wa dunia ya kwanza."

Anafafanua kuwa kwa muda wa miaka 23, amekuwa akiandaa mpango huo na kwamba anaendelea kuuboresha, ili usaidie kuifanya Tanzania kujikomboa katika nyanja ya elimu, sayansi na teknolojia.

Mdau huyo anasema alishatuma nakala ya waraka wake kwa viongozi na wataalamu wote ili wausome na kuufanyia kazi kwa manufaa ya nchi na vizazi vilivyopo na vitakavyofuata.

Ndimubansi ambaye ni mstaafu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa TMA na mkazi wa mtaa wa Mbwate Kibaha Mjini mkoani Pwani, anasema Tanzania inaweza kupiga hatua zaidi za kimaendeleo kupitia diplomasia ya elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Anasema katika uumbaji, Mungu aliumba mikono miwili, miguu miwili, macho mawili na watu ni mume na mke vitu vyenye uhai na visivyo na uhai.

"Anasema Mungu aliumba mifumo miwili ili itumike kuendeleza nchi, na mataifa yaliyoendela kiviwanda ikiwamo Marekani, Ulaya, China, Japan, Korea Kusini, Malyasia na Singapore, zina mifumo ya diplomasia ya elimu ya masomo ya sayansi, teknolojia na ubunifu."

> Lakini ninaamini kwamba umefika wakati sasa kwa Tanzania kuwa na diplomasia ya pili ambayo itajikita katika kuwekeza kwenye ubunifu ili nasi tutengeneze vitu vyetu.

"Mkono wa kulia una jukumu la kuunda mitambo mbalimbali na wa kushoto ni kuuza bidhaa zinazozalishwa na viwanda ambavyo vimetengezwa na mkono wa kulia," anasema.

Anasema ndio msingi wa ujeuri wa utajiri wa nchi hizo ambazo chimbuko lake ni diplomasia ya mfumo wa elimu ya masomo ya sayansi, teknolojia na ubunifu inayolenga kuinua uchumi wao.

### VYUO NA UTAFITI

"Kinachotakiwa kwetu ili diplomasia hiyo ifanikiwe, ni kuanzisha vyuo vingi ambavyo vitatoa elimu ya ufundi wa fani mbalimbali, ili kuwaandaa vijana wetu kuwa wataalamu wabobezi," anaongeza mtaalamu huyo.

Tanzania kwa sasa ina diplomasia ya uchumi na kwamba kuna haja ya kuwa na diplomasia na elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu, ili zote zifanye kazi kwa manufaa ya Watanzania.

"Ikumbukwe kuwa hata mitambo inayotumika katika shughuli mbalimbali inatoka nje, ikiharibika hata nati na bolti inabidi kuita wataalamu kutoka nje na kutengeneza kwa gharama kubwa," hivi kuna haja ya kuendelea na hali hiyo? Anahoji Ndimubansi.

Anasema ili kuepuka hayo, ni taifa liwe na diplomasia ya elimu ya masomo ya sayansi kwa kuwekeza katika vyuo vya kutosha na masuala ya teknolojia ili Tanzania iweze kuunda, mitambo, magari, ndege na vitu vingine ambavyo vimekuwa vinunuliwa kutoka nje.

"Nimeandika maelezo kwa kirefu kuhusu diplomasia hii. Ingawa nimesambaza andiko langu kwa mawaziri, ninatamani nionane na Rais nimweleze kwa kina kwa nini nimekuja na wazo hili muhimu wake kwa maendeleo ya taifa," anasema.

### KUJIKOMBOA

Ndimubansi anasema diplomasia hiyo inaweza kuwa mpango wa kuifanya Tanzania na Afrika kwa ujumla kujikomboa katika nyanja ya elimu, sayansi na teknolojia na kuacha utegemezi ambao umedumu kwa miaka 60.

"Mbali na kuunda na kutengeneza vitu vikubwa na vya kisasa kwa juhudi zetu wenyewe, mfumo wa diplomasia ya elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu unaweza kusaidia kuwa na viwanda mama vitakavyounda mashine kutokana na vyuma vitakavyotengeneza mashine mbalimbali za mawasiliano zikiwamo redio, simu na vitu nyingine tunavyo hapa nchini kwani tuna madini, makaa yam awe, chuma, shaba na bati pia," anasema Ndimubansi.

### DIPLOMASIA MBILI

Anasisitiza umuhimu wa nchi kuwa na diplomasia za aina mbili ikiwamo ya uchumi iliyopo sasa, kwa maelezo kuwa kwamba ni mojawapo ya kulikomboa taifa kutoka kwenye utegemezi uliodumu kwa miongo mingi.

Kuhusu diplomasia ya uchumi anasema ni moja ya mambo yanayotiliwa mkazo na serikali, huku wawakilishi wa Tanzania nje ya nchi wakiimarisha diplomasia hiyo.

"Wawakilishi hao wakiwamo mabalozi, wanakuwa na jukumu la kutangaza na kujibu maswali kutoka kwa watu wa nje wanaotaka kuja kutembelea Tanzania ili kujionea vivutio mbalimbali," anasema hivyo ni jambo jema.

Aidha, anasema dhana ya diplomasia ya uchumi inagusa uwakilishi wa Tanzania nje ya nchi ambao unajikita kwenye mambo yanayohusisha zaidi uchumi, ikiwamo uwekezaji na biashara kwa nchi ambayo inajishughulisha kiuchumi na mataifa mengine.

"Hayo yote ni mambo mazuri. Lakini ninaamini kwamba umefika wakati sasa kwa Tanzania kuwa na diplomasia ya pili ambayo itajikita katika kuwekeza kwenye ubunifu ili nasi tutengeneze vitu vyetu," anasema.

Ndimubansi anaeleza kuwa kati ya mambo ya muhimu katika diplomasia ya uchumi ni kuvutia uwekezaji kutoka nchi mbalimbali, na hata kiwa na wataalamu wa nje, kuna haja ya Tanzania nayo kuwa na wataalamu wake.

"Malighafi ya kuunda na kutengeneza vitu mbalimbali ipo, lakini tunakosa wataalamu, hivyo tukiwa na diplomasia ya elimu inayohusu ubunifu, tutakuwa nao wa kutosha," anasisitiza.

RAIS MPYA BOLA TINUBU

# Kiongozi aliyechaguliwa kwa kura kiduchu zaidi tangu mwaka 1999

• Kuongoza nchi yenye watu mafukara milioni 99



Bola Tinubu sasa ndiye Rais wa Nigeria. **PICHA: AFP**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Nigeria, Bola Tinubu (71), ameanza kazi rasmi baada ya kuapishwa kuwa kiongozi wa taifa hilo lenye watu wengi zaidi ya milioni 120 hapa barani Afrika, anapotinga Ikulu jijini Abuja anakutana na changamoto lukuki.

Bola Tinubu, Gavana wa zamani wa jiji la Lagos ambalo ni kitovu cha uchumi Nigeria amechukua mikoba kutoka kwa mstaafu Rais Muhammadu Buhari, akitarajiwa kuiongoza nchi hiyo kwa miaka nane yenye mihula miwili ya miaka minne kila mmoja.

Ni rais wa 16 alitawazwa juzi Jumatatu Mei 29, akitarajiwa kuliongoza taifa la tatu kwa kuwa na wingi wa watu Afrika itakapofika mwaka 2050, katika hotuba yake kiongozi huyo mwenye miaka nane inayomsubiri kuongoza taifa hilo anaahidi kuendeleza juhudi za Buhari za kudumisha demokrasia katika nchi inayokabiliwa na mizozo mingi ya kiusalama hasa mashambulizi ya kundi la waasi wa Boko Haramu, umaskini, vita vya kikabila, vita vya wakulima na wafugaji, ugomvi wa kidini, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana na njaa.

Tume ya uchaguzi Nigeria, ilimtangaza kuwa mshindi katika uchaguzi uliofanyika mapema mwaka huu Februari 25, 2023, akishinda kwa kura milioni 8.8 licha ya Nigeria kuwa na watu takribani milioni 120.

> Kutokubalika, ni asilimia 37 tu ya wapiga kura walimuunga mkono Tinubu, hivyo kumfanya kuwa Rais wa Nigeria aliyechaguliwa kwa kura chache zaidi tangu mwaka 1999.

Bila kujali kesi zinazoendelea mahakamani zikifunguliwa na vyama vya upinzani kikiwamo cha mpinzani wake mkuu Atiku Abubakar wa chama cha PDP aliyepata kura milioni 6.9 ambaye anaungwa mkono na Rais mstaafu Olusegun Obasanjo, aliyefuatiwa karibu na Peter Obi wa chama cha Labour aliyeibuka na kura milioni 6.1 na kushangaza mamilioni ya Wanaigeria, Tinubu anaahidi kuwaunganisha Wanigeria.

Akisema ilani yake ya "matumaini mapya" inatoa vipaumbele katika kutengeneza nafasi za kazi za kutosha na kuongeza uzalishaji wa bidhaa za ndani, uwekezaji kwenye kilimo na miundombinu ya umma na kubadilisha sura ya Nigeria.

Vipaumbele vingine vinahusisha kutoa nafasi za kiuchumi kwa watu maskini pamoja kuwa na mfumo bora wa usalama wa taifa ili kukabiliana na changamoto zote za kiusalama, inaripoti DW.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wanasema ahadi na matumaini yaliyotolewa na Tinubu yanakumbusha kile alichoahidi Buhari alipochaguliwa kuwa rais mwaka 2015. Vipaumbele vyake navyo vilijikita katika kupambana na vitisho vya usalama na kuukuza uchumi lakini aliishia kushindwa kufikia matarajio ya walio wengi.

Rais Samia Suluhu Hassan, ni miongoni mwa waliohudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais Bola Tinubu akiungana na viongozi wengine wa Afrika akiwamo Rais wa Afrika ya Kusini, Cyril Ramaphosa, Paul Kagame wa Rwanda, Nana Akufo-Addo wa Ghana na wawakilishi wa Marekani, Uingereza na China.

Anamrithi rais mstaafu aliyeingia madarakani Mei 2005, Buhari baada ya kumshinda Goodluck Jonathan katika uchaguzi mkuu, kiongozi huyo alizaliwa Desemba 1942 ni mwanachama wa Chama cha All Progressive Congress APC, ambacho ndicho cha Tinubu na ndiye aliyemteua.

Kwa mujibu wa BBC Swahili Nigeria inayojulikana kama "jitu kubwa la Afrika", kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu na uwezo wake wa kiuchumi, ni taifa lenye matatizo makubwa yatakayomkabili Bola Tinubu anapochukua wadhifa wa rais, inaeleza kuwa huenda asifadhaike na changamoto hizo.

Kama gavana wa mara mbili wa Lagos, alifufua kituo cha kibiashara cha Nigeria na kwamba sio kazi rahisi na anafahamu vyema masuala hayo, lakini Wanaigeria, hata wale ambao hawakumpigia kura, watataka kuona matokeo ya makubwa kutoka kwa Tinubu.

Inataja baadhi ya vikwazo vikubwa anavyokabiliana navyo na jinsi anavyoweza kukabiliana navyo kuwa ni pamoja na kukomesha ruzuku ya mafuta, jambo lililopigwa na serikali zilizofuata tangu kuanzishwa kwake miaka ya 1970.

Licha ya utajiri wake wa mafuta, Nigeria haiwezi kusafisha mafuta ghafi ya kutosha kukidhi mahitaji ya ndani hivyo inaagiza bidhaa za petroli kutoka nje, ambazo zinauzwa kwa bei iliyowekwa na serikali. Kwa vile hii kawaida huwa chini kuliko bei ya kuagiza, serikali hulipa tofauti hiyo, inasema BBC.

Inaongeza kuwa ruzuku hiyo inaleta madhara katika kufifia kwa fedha za umma, mwaka jana iligharimu Naira 4.3 sawa na Dola 9.3 bilioni na kwa nusu ya kwanza ya mwaka huu, Naira 3.36 trilioni zilitengewa bajeti.

Kutokubalika, ni asilimia 37 tu ya wapiga kura walimuunga mkono Tinubu, hivyo kumfanya kuwa Rais wa Nigeria aliyechaguliwa kwa kura chache zaidi tangu mwaka 1999.

Alishinda uchaguzi uliokuwa na ushindani mkali ambao ulifichua migawanyiko ya kikabila na kidini ambayo imedumu hata katika miji ya Nigeria yenye watu wengi zaidi duniani na kwamba atalazimika kufanya usawa wakati wa kuchagua serikali yake kujenga madaraja katika mgawanyiko huu.

Kuna dalili kwamba tayari anafanya hivyo, inasemekana alikutana na wanasiasa wawili wa upinzani tangu kushinda kura ya Februari ili kuweka mambo sawa, inasema BBC.

Kurekebisha uchumi ni kigingi kingine, Wanaigeria wengi wanakubali kwamba hili ni eneo la utaalamu la Tinubu lakini mambo hayajawahi kuwa mabaya zaidi kwa Nigeria kama ilivyo sasa kwani mmoja kati ya watatu hana ajira, mfumuko wa bei uko kwenye rekodi ya asilimia 22 na watu milioni 96 wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa dola 1.90 (takribani Shilingi 5,000) kwa siku.

Utekaji nyara na ukosefu wa usalama ni janga jingine linalomkabili Tinubu analohitaji kulishughulikia haraka, kutokana na ukubwa wa tatizo. Utawala wake utakuwa ukikabiliana na wahalifu wenye silaha wanaoendesha pikipiki kaskazini-magharibi, utekaji nyara wa nchi nzima na kundi lenye vurugu la kujitenga kusini-mashariki.

Mapigano mabaya kati ya wakulima na wafugaji pia yanaendelea katika majimbo ya kati, wakati wa kampeni za uchaguzi, Naibu Rais anayetoka Kusini, Kashim Shettima, anasema hilo litakuwa jukumu lake akisifu uzoefu wake kama gavana wa jimbo la kaskazini-mashariki la Borno, ambalo ni makazi ya vikundi vingi vya wapiganaji wakiwamo waasi wa Boko Haram, inaripoti BBC.



## Wazalishaji hewa ukaa watakiwa kutoa elimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamza Khamisi, amewataka wadau wa uzalishaji wa hewa ya ukaa kutoa elimu kwa jamii namna ya biashara hiyo inavyofanyika pamoja na fursa zilizopo.

Alitoa agizo hilo wakati wa hafla ya upandaji miti 1,000 iliofanyika mwishoni mwa wiki katika Shule ya Sekondari ya Buigiri iliopo Chamwino mkoani Dodoma.

Wakati huohuo watekelezaji wa mradi wa Tabora Carbon Cradit wanatarajia kuvuna hewa ya ukaa cubic tani 1.5 bilioni ndani ya miaka 30 ijayo ili kuhakikisha uhifadhi wa misitu unakuwa endelevu hapa nchini na kuwanufaisha wananchi.

Kadhalika, aliwataka wadau hao kuwapa elimu jamii ya namna ya uvunaji wa hewa ya ukaa lakini kuwasisitiza katika suala zima la utunzaji misitu pamoja na mazingira.

Alisema dunia ya sasa imekumbwa na jangwa kubwa la uharibifu wa mazingira na magonjwa mengi yanatokanayo na athari za mazingira zinazochangiwa na mabadiliko ya tabia nchi, hivyo jamii ikiwa na elimu ya utunzaji misitu na mazingira itasaidia kuepuka kuharibu mazingira.

"Nawapongeza taasisi hii kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kutunza mazingira hii isiishie Dodoma iende na mikoa mingine hapa nchini ikiwamo ya bara na visiwani," alisema visiwani.

Pia aliwataka kuielimisha jamii kuhusiana na uzalishaji wa hewa ya ukaa ikiwamo fursa zinazopatikana jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa jamii kuacha kuharibu mazingira ovyo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Livingway (URT) Limited, Dk. Ernest Irungu, alisema utekelezaji wa mradi huo wanafanya kwa ushirikiano na serikali kupitia Wakala wa Misitu Tanzania TFS.

Mkurugenzi huyo alifafanua zaidi ya kuwa malengo waliyonayo ni makubwa na ili kufikia hatua hiyo watakuwa na menejimenti endelevu ambayo itahakikisha hawatashuka kiwango kwenye utunzaji wa misitu na mazingira ili kuwezesha uhifadhi wa misitu kuwa endelevu.

"Tutakuwa na menejimenti endelevu ambayo itakuwa ikiangalia kwa karibu namna ya utunzaji misitu kwa kushirikiana na serikali kupitia TFS, ili kuhakikisha jamii inanufaika ikiwamo kuinuka kiuchumi," alisema Dk. Irungu.

Alisema kutakuwa na ufugaji wa nyuki pamoja na mnyororo wa thamani ndani yake ambao utawawezesha vikundi mbalimbali vya ushirika, watu binafsi pamoja na wao kwenda kuweka mizinga katika misitu ambayo itakuwa imehifadhiwa na baadaye kuvuna asali.

"Hii ni moja ya fursa ambazo wananchi watanufaika nazo kupitia uzalishaji wa hii hewa ya ukaa hapa nchini, lakini fursa hiyo itaifanya jamii isiendelee kukata misitu kwa sababu watakuwa na shughuli mbadala ya kufanya," alisema Dk. Irungu.

Alisema watakuwa pia na miradi endelevu ya kilimo ambayo itawanufaisha wakazi wa maeneo hayo kuendesha kilimo endelevu cha mazao ya matunda na biashara ambayo yatakuwa yakichakatwa ili kuwekwa katika mnyororo wa thamani.

# Mbunge ahoji taasisi za fedha kuacha kuwakopesha wakulima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kutoa tamko kwa taasisi za fedha ambazo zimeacha kuwapatia mikopo wakulima baada ya serikali kuanza kutoa ruzuku ya pembejeo.

Akiuliza swali la nyongeza jana bungeni, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema baada ya serikali kuanza kutoa ruzuku kuna baadhi ya taasisi zimeacha kutoa mikopo iliyokuwa ikisaidia gharama za matayarisho ya mashamba na uvunaji.

"Changamoto zinazokabili mazao ya mkakati zingeweza kutatuliwa na mfuko wa maendeleo ya kilimo. Je, lini mfuko huu utaanza?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema serikali pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wamekaa na taasisi za kifedha kujadiliana jambo hilo huku akibainisha baadhi ya kero zilizojitokeza ikiwamo ya urejeshaji wa mikopo ambayo ilitokana na wakulima wengi kutosajiliwa.

Kwa sasa, alisema wakulima wengi wameshasajiliwa na kila mkulima atatambulika shamba lake lilipo, ukubwa wa shamba lake ili kumrahisishia taasisi za fedha namna bora ya kumpatia mkopo mkulima.

"Naamini katika hili wakulima wengi watapata mikopo kupitia taasisi za kifedha," alisema.

Akizungumzia kuhusu mfuko wa maendeleo ya kilimo, Mavunde alisema umeshaanza kufanya kazi na kwamba muda si mrefu watapata vyanzo vya kuutunisha ili wakulima wanapopata vikwazo wapate huduma.

Katika swali la msingi, Mbunge Chikota alihoji serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wakulima wa korosho wanapata mikopo ili waweze kugharamia kilimo cha korosho.

Mavunde akijibu swali hilo, alisema serikali kupitia Tume hiyo inaratibu uwezeshaji wa wakulima wa korosho kupata mikopo ya kuendeleza zao la korosho ikiwamo pembejeo na utunzaji wa mashamba.

Alisema uwezeshwaji huo utafanyika kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika kwa kuweka dhamana wakulima ili kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha.

"Aidha, serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye riba nafuu kuanzia asilimia tisa kushuka chini," alisema.




Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati), akishuhudia utiaji saini wa ujenzi wa mradi wa umeme kwa kutumia nishati ya jua wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 150, utakaogharimu Sh. bilioni 274.76 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Maharage Chande (wa pili kulia) na Mwakilishi wa kampuni ya Sinohydro Corporation Shi Yong jijini Dodoma juzi. **PICHA PAUL MABEJA**

# Mradi umeme jua kuzalisha megawati 150 wasainiwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limesaini mkataba wa ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua kwa mara ya kwanza nchini wenye uwezo wa kuzalisha megawati 150, utakaogharimu Sh. bilioni 274.76.

Mradi huo utatekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza zitazalishwa megawati 50 na awamu ya pili itahusisha uzalishaji wa megawati 100.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema hayo jana jijini hapo, baada ya kushuhudia utiaji wa saini utekelezaji wa mradi huo kati ya TANESCO na mkandarasi wa mradi huo Sinohydro Corporation kutoka China.

"Huu ni mradi mkubwa kuwahi kutokea wa kuzalisha umeme kwa kutumia jua hapa nchini na katika Ukanda wa Afrika Mashariki," alisema Makamba.

Aidha, alisema kusainiwa kwa mradi huo ni sehemu ya mipango ya mapinduzi katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mseto katika sekta ya nishati nchini ili kufikia lengo la kuwa na megawati 5,000 kwenye gridi ya taifa ifikapo 2025.

"Kwa mara ya kwanza tunakwenda kuingiza umeme utokanao na nishati ya jua kwenye gridi ya taifa hii ilikuwa ni ndoto ya muda mrefu sana na sasa inakwenda kutimia chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, lakini pia lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa kunakuwapo na vyanzo mseto ili chanzo kimoja kinapo pata shida kingine kinatibu tatizo," alisema.

Kadhalika, aliiagiza TANESCO kubainisha maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya uzalishaji wa umeme jua na upepo ili zinapopatikana fedha utekelezaji wake uanze mara moja.

"Ujenzi wa miradi ya umeme kwa kutumia jua na upepo ni nafuu kuliko chanzo kama vile maji au gesi gharama zake ni kubwa na zinatumia muda mrefu kukamilika," alisisitiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema utekelezaji wa maradi huo unatarajiwa kuanza Juni 2023, ambapo utachukua miezi 14 hadi kukamilika kwake.

"Awamu ya kwanza itaanza na uzalishaji wa megawati 50 na gharama zitakazotumika ni Sh. bilioni 92.5 na awamu ya pili ambayo itazalisha megawati 100 itagharimu kiasi cha Sh. bilioni 174.5 na fedha hizi zote ni za serikali ambazo imeomba mkopo kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa la AFD," alisema Chande. Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema wanaishukuru serikali kwa mradi huo ambao unakwenda kujibu kero ya kukatika kwa umeme katika mkoa wake.

"Tunaishukuru sana serikali mradi huu utakuwa msaada mkubwa sana katika kujibu kero za kukatika kwa umeme Shinyanga kwani mahitaji yapo mengi hasa katika migodi na matumizi mengine," alisema Mndeme.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Judith Kapinga, aliitaka TANESCO kumsimamia mkandarasi ili akamilishe mradi huo kwa wakati na kwa viwango vilivyopangwa ili uwe na tija kwa taifa.





# Shule ya wasichana yakabiliwa na uhaba wa majisafi, vyoo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHULE ya Sekondari ya Wasichana Manyunyu iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Mkoa wa Njombe inakabiliwa ukosefu wa majisafi na salama, vyoo hali iliyosababisha watoto wa kike kushindwa kujisitiri wakati wa hedhi.

Tatizo hilo limeibuliwa baada ya mwanamitindo, mwasisi na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Flaviana Matata Foundation na Lavy Pads, Flaviana Matata alipotembelea shule hiyo ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani.

Alisema katika sekondari hiyo wamebaini matatizo kadhaa ikiwamo ya maji na vyoo, hivyo watahakikisha wanatatua suala hilo.

Alisema kupitia taasisi hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na wadau wengine wataboresha miundombinu ya maji, vyoo na sehemu ya kuchomea taulo (pedi) zilizotumika katika maeneo ya shule ili kuwa na mazingira rafiki kwa wanafunzi wa kike na kufikia lengo la hedhi salama kwa wote.

"Leo ni Siku ya Hedhi Salama Duniani, hedhi ni tunu ni hatua muhimu kwa mtoto wa kike kujiandaa kuwa mama, kwa hiyo najua ni jambo linaloongelewa kwa usiri lakini ni jambo la kujivunia ni jambo la msingi sana," alisema Flaviana.

Aliongeza kuwa bado kuna tatizo kwa baadhi ya jamii kuhisi hedhi ni jambo la aibu hivyo ni wakati wa kutoa elimu ili wanawake waone hedhi ni tunu na heshima.

Ofisa Miradi wa Tasisi Flaviana Matata, Suzan Cleopas, alisema takribani wanafunzi 800 katika Shule ya Sekondari Manyunyu wamepewa pedi huku zoezi hilo likiambatana elimu ya hedhi salama. Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Charles Meshack, alisema elimu waliyoipata wanafunzi wanaamini itawasaidia kijitambua, kuongeza ufaulu na kujiamini.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Manyunyu, Noel Mtweve, alisema ni kweli kuna tatizo la miundombinu ya vyoo na maji hasa katika shule zilizopo vijiji, hivyo anapongeza Taasisi ya ya Flaviana Matata kuzipa kipaumbele shule za pembezoni mwa mji.

Mwanafunzi Mariam Patrick wa kidato cha sita Shule ya Sekondari Manyunyu, alisema bado kuna baadhi ya wazazi hawatambui umuhimu wa taulo za kike hali inayosababisha kutoona umuhimu kuwanunulia.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mratibu wa Mradi Shirikishi wa Wasindikaji na Wazalishaji wa Maziwa (TI3P) unaoratibiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Joseph Mabula (kulia), alipotembelea banda la benki hiyo katika maonyesho ya Wiki ya Maziwa mkoani Tabora. TADB kwa kushirikiana na wadau wengine wanatekeleza mradi wa T13P unaolenga kuwanufaisha wafugaji wadogo 100,000 wa ng'ombe wa maziwa na wachakataji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chongolo amwagiza Bashe kukagua bwawa la samaki

**Na Nebart Msokwa,** IRINGA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amemwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kwenda kukagua Bwawa la Samaki la Masaka lililoko katika Wilaya ya Iringa ambalo litatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Aidha ameiagiza Tume ya Umwagiliaji nchini, kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika eneo hilo ili kuwasaidia wananchi wa eneo hilo kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kukagua bwawa hilo pamoja na kupanda vifaranga vya samaki 3,000 ambapo alimtaka Waziri Bashe kutekeleza agizo hilo ndani ya wiki tatu ili faida ya bwawa hilo ianze kuonekana

Alisema Wizara ya Maji imefanya kazi kubwa ya kusimamia ujenzi wa bwawa hilo lakini ili kuendeleza kilimo inatakiwa Wizara ya Kilimo nayo kuweka mkazo.

"Hapa kuna kosa lilifanyika tangu mwanzo, watu wa Tume ya Umwagiliaji hawakushirikishwa maana wangekuwa wameliona andiko wangekuja mapema hapa, sasa nitaongea na Waziri wa Kilimo aje hapa ndani ya wiki tatu akiwa na wataalamu wake," alisema Chongolo.

Aliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kuhifadhi mazingira kwenye bwawa hilo kwa kupanda miti ili maji yanayovunwa yadumu kwa muda mrefu pamoja na kuvutia watalii kwenye eneo hilo.

Alisema miti inayotakiwa kupandwa kwenye eneo hilo ni ya matunda, kivuli pamoja na mianzi kwa ajili ya kuhifadhi mila na desturi za wenyeji wa eneo hilo hasa utengenezaji wa pombe za kienyeji aina ya ulanzi.

Diwani wa Kata hiyo, Mathew Nganyagwa, alisema bwawa hilo limejengwa na serikali kwa ajili ya kutatua shida ya maji ambayo imekuwa ikiwakabili wananchi wa eneo hilo kwa muda mrefu.

Alisema mbali na ufugaji wa samaki pia bwawa hilo linatarajiwa kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwenye mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 1,000 na hivyo kuwasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao.

Alisena wananchi wa eneo hilo wamekuwa wakizalisha mazao kwa kiwango kidogo kutokana na kulima kilimo cha kutegemea mvua na hivyo endapo watawekewa miundombinu ya umwagiliaji wataongeza uzalishaji.

"Hili bwawa pia tutalitumia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa sababu eneo letu tunakabiliwa na tatizo la uhaba wa maji, kinachotusumbua ni watu wa Tume ya Umwagiliaji hawajawahi kufika hapa," alisema Nganyagwa.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Iringa, Calvin Ndege, alisema bwawa hilo limejengwa kwa Sh. bilioni 1.5 ambazo zilitolewa na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Maji.

Alisema bwawa hilo lina uwezo wa kuchukua zaidi ya lita za ujazo 439.8 na kwamba maji hayo yana uwezo wa kutunzwa kwenye bwawa hilo kwa kipindi cha mwaka mzima bila kukauka.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema ili kurahisisha usafirishaji wa mazao mbalimbali yatakayokuwa yanazalishwa na wananchi kwenye eneo hilo, ofisi yake itashirikiana na wadau mbalimbali kuboresha miundombinu ya barabara.

## CCM kuanza kusajili wanachama kielektroniki

**Na Nebart Msokwa,** IRINGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinaandaa kadi za kisasa za kielektroniki kwa ajili ya wanachama wake ambazo zitawawezesha kupata huduma mbalimbali za kijamii.

Katibu wa Oganizesheni wa CCM, Issa Haji Ussi, aliyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Kising'a Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

Mkutano huo ulikuwa ni mwendelezo ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, katika mkoa huo yenye lengo la kusikiliza kero za wananchi, kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho pamoja na kuangalia uhai wa chama hicho tawala.

Gavu alisema kadi hizo za kisasa zitawasaidia wanachama kupata zaidi ya huduma 10 zinazotolewa na taasisi mbalimbali za kiuchumi na kijamii zinazotolewa nchini.

Alizitaja baadhi ya huduma ambazo wananchi watakuwa wanazipata kwa kutumia kadi hizo kuwa ni pamoja na bima ya afya, mifuko ya hifadhi za jamii na huduma za kibenki ambapo zitatumika kama kadi za kutolea fedha (ATM).

Alisema kadi za awali ambazo zilitengenezwa zilibainika kuwa na upungufu hasa kutoendana na wakati huu wa maendeleo ya teknolojia na hivyo wakaamua kusitisha kuzitoa ili ziboreshwe kwanza.

"Kadi zetu mpya za kisasa zitaanza kutolewa Agosti, kwa hiyo nawaomba wanachama wa CCM mwendelee kukiamini chama chenu na kuendelea kuzilipia hizi kadi," alisema Gavu.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuwa na msimamo hasa vijana ili wasirubuniwe na baadhi ya vyama ambavyo vinawapa matumaini hewa.

Katibu Mkuu wa CCM, Chongolo aliwataka viongozi wa chama hicho katika ngazi zote kuendelea kutafuta wanachama wapya ili kuendelea kukiimarisha chama.

Chongolo aliwataka wanachama wa chama hicho kutojibu mashambulizi pale wanapotukanwa na vyama vya upinzani na badala yake waitumie miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali kuwajibu.

Alisema serikali imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maendeleo hasa katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara pamoja na sekta ya kilimo na hivyo akaeleza kuwa miradi hiyo inatosha kuwajibu wapinzani wanaoikosoa serikali.

Alisema lengo la chama hicho ni kuendelea kushika dola na hivyo lazima kifanye kazi ya kuwaletea wananchi maendeleo, ili waendelee kukiamini na kukichagua kwenye chaguzi mbalimbali.

"Kuna baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani wao kazi yao ni kutukana matusi, sasa sisi hatuwajibu kwa matusi na badala yake tunawajibu kwa kutekeleza miradi ya maendeleo, wakitukana waonyeshe shule, waonyeshe vituo vya afya na barabara," alisema Chongolo.

Mbunge wa Isimani, William Lukuvi, alisema katika jimbo lake wananchi wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la uhaba wa maji kwa muda mrefu, lakini kwa sasa tatizo hilo limepungua kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Alisema kwa sasa asilimia kubwa ya wananchi wanapata maji ya bomba na maeneo machache yaliyobakia wanaendelea na utekelezaji wa miradi itakayomaliza kabisa tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego alisema kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji mkoani humo ni nzuri kwa maelezo kuwa maeneo ya mjini upatikanaji wa huduma hiyo ni asilimia 84 na vijijini ni asilimia 74.





# Serikali kuwawezesha vijana kuwa wajasiriamali

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

KATIKA kutokomeza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, imesema imejipanga kuwawezesha vijana kujitegemea na kuwa wajasiriamali.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Tabia Maulid Mwita, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023-2024 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema baraza la vijana ndiyo chombo halali ambacho kazi yake kubwa ni kuwaunganisha vijana wote bila ya kujali tofauti za itikadi za kisiasa kwa ajili ya kuwawezesha kuwa wajasiriamali kwa kuibua miradi ya uzalishaji mali na uchumi.

Alisema miongoni mwa mikakati ya Serikali ya Zanzibar ni kuwajenga vijana kuondokana na mawazo kwamba ajira pekee ni zile zinazotoka serikalini ambapo mkazo umewekwa katika kazi za ujasiriamali ikiwamo katika sekta ya kilimo na ufugaji pamoja na mazao ya baharini.

Alisema kupitia miradi katika baraza la vijana mkazo umewekwa zaidi katika kuibua miradi ya kilimo cha mazao ya viungo ambayo yamebainika kuwepo kwa soko la uhakika na kipato.

Waziri huyo alisema baadhi ya asasi za kiraia zimejikita katika kuwaendeleza vijana katika kilimo cha viungo pamoja na Jumuiya ya Ulaya (EU) katika kuwahamasisha wakulima kulima kilimo cha vanila.

Aidha, alisema tayari vikundi vya vijana 285 vya kiuchumi vimeibuliwa Unguja na Pemba na kupatiwa mikopo kwa ajili ya kazi za ujasiriamali pamoja na kupatiwa msaada wa kiufundi wa elimu.

Alisema tayari mikopo ya Sh.milioni 669.5 imetolewa kupitia baraza la vijana nchini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kiuchumi na maendeleo.

Kadhalika, aliwataka wajasiriamali ikiwamo wanawake kujitokeza kuchangamkia fursa za mikopo zinazotolewa kupitia mazao ya baharini ikiwamo mwani na matango bahari na shughuli za ufugaji wa samaki.

Alisema zaidi ya wakulima wafugaji wa samaki pamoja na mwani 2,000 wamepatiwa mafunzo na wengine kutembelea China kwa ajili ya kupata mbinu za kisasa za kilimo cha mwani chenye tija kinachotokana na usarifu wa bidhaa mbalimbali.

Alisema serikali inaendelea na mikakati yake ya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili katika kiwango cha kimataifa kupitia Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki (KAMAKA).

Waziri Tabia alisema juhudi zimeanza kuchukuliwa kuona kwamba taasisi mbalimbali zinatumia lugha ya Kiswahili katika kufanya machapisho yake pamoja na kutoa taarifa zake ikiwamo hukumu katika Mahakama kwa kutumia lugha ya Kiswahili.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza mwandishi wa habari mwandamizi, Salim Said Salim (kushoto), alipozungumza na wahariri, waandishi wa habari, Ikulu jijini Zanzibar jana, kuhusu ziara yake ya nchini Qatar hivi karibuni. **PICHA: IKULU**

## ...Yakiri uwapo tatizo uhaba wa nazi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema serikali inatambua tatizo lililopo la uhaba wa nazi, kwamba eneo la kilimo cha minazi limepungua kutoka hekta 22,000 hadi hekta 16,000.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Kojani Haasan Hamad, aliyetaka kujua endapo serikali inafahamu uwapo wa uhaba wa zao hilo visiwani humo.

Shamata alisema uzalishaji wa nazi umepungua kwa zaidi ya asilimia 35 kutoka wastani wa nazi 120,000,000 hadi nazi 75,000,000, kwamba sababu kuu ni kasi ndogo ya uoteshaji na uhudumiaji.

Alisema sababu zingine ni wizi wa nazi na madafu, ukataji ovyo wa minazi na kuwapo kwa biashara kubwa ya madafu.

"Wizara yangu imechukua juhudi za kukamilisha mpango mkakati wa uendelezaji wa nazi wa miaka mitano kuanzia 2023 hadi 2027," alisema.



Aidha alisema mpango huo umeweka lengo la kuotesha miche laki tatu ya minazi na kuigawa bure kwa wananchi kila mwaka.

Alisema kwa mwaka huu tayari miche 45,000 ipo katika utaratibu kutoka vitalu vya watu binafsi (33,000) na vitalu vya serikali (12,000).

# Mfumo wa kurahisisha huduma za kitalii wazinduliwa

Na Mwandishi Wetu

SEKTA ya utalii imepata ahueni katika kuhudumia watalii baada ya kampuni ya Tempo Africa kuanzisha mfumo wa kuhudumia watalii wa ndani na nje ya nchi kwa kutumia 'application' maalumu itakayowawezesha watalii kupata huduma tofauti kwa pamoja.

Mfumo huo mpya unawawezesha watalii kuagiza na kupata bidhaa na huduma.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na huduma hiyo mpya, Mkurugenzi Mtendaji wa Tempo Africa, Pendo Lema, alisema kuwa kufuatia pengo la kuhudumia wageni na tatizo linalohusiana na huduma mbalimbali wanazopata katika sekta hiyo, kampuni hiyo iliamua kuja na ufumbuzi wake kupitia huduma hiyo mpya.

"Ubunifu wetu umejikita zaidi katika kuboresha huduma bora za kukodisha nyumba, usafiri wa aina mbalimbali, huduma ya tiketi za ndege na huduma zingine za utalii kwa ujumla," alisema.

Alisema kuwa kampuni ya Tempo Afrika ambao ni watoa huduma ya utalii inayoaminika katika kutoa huduma zake mbalimbali inawapa wateja wetu mikataba bora na yenye masharti nafuu.

Hivyo, aliwahakikishia watalii wanaokuja nchini kwamba watapata huduma nzuri, salama na za uhakika zikiwamo zile za kutembelea maeneo ya utalii ya kihistoria hapa nchini.

Alisema pia watapata usafiri bora kwa gharama nafuu na kupitia huduma za magari, huduma ya kuhifadhiwa vyumba vya malazi kwenye hoteli, huduma ya tiketi za ndege na mawasiliano.

Kuhusu 'application' ya simu za mkononi, alisema kwa sasa watumiaji wanaweza kupata huduma kuhusu nyumba za kupanga, hoteli na nyumba za wageni mbalimbali.

Alisema hatua hiyo ya ubora wa huduma hizo inalenga katika kuchangia juhudi za serikali katika kutangaza utalii wa Tanzania kama miongoni vya vituo muhimu vya utalii na vyenye ubora.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kutangaza utalii kupitia Filamu ya Royal Tour ambayo sasa ni maarufu katika nchi nyingi; tunataka watalii wawe na wakati mzuri kwa kupata huduma nzuri na zenye unafuu kwa rahisi kupitia huduma za simu zao za viganjani wakiwa nyumbani," alisema.

Alisema kampuni yake iko tayari kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuhakikisha watalii wanapata huduma ziakazowafanya waikumbuke Tanzania na kuifanya kama kituo cha bora cha utalii watakachokitembelea mara kwa mara.

Hivyo, alitoa wito kwa Watanzania kutumia vyema huduma hiyo mpya kupata huduma na bidhaa mbalimbali za utalii ambazo ni pamoja na kupangisha nyumba za kuishi jambo ambalo kwa sasa ni kero kubwa kwa Watanzania wengi.

Alisema Tempo Africa ilianzishwa mwaka 2021 na imesajiliwa nchini Tanzania.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Registration of Documents Act,Cap.117 R.E. 2019)**

**1,ANNAMARY AUGUSTINO KOMIE** of P. O.BOX 30, MBINGA formerly known as **ANAMARY KOMIYE** ,do hereby absolutely renounce the use of my former name, **ANAMARY KOMIYE** and in lieu thereof to assume as from the date hereof the name of **ANNAMARY AUGUSTINO KOMIE AND IN PURSUANCE** of such change of name as aforesaid I, hereby declare that I shall at all time hereafter in all records deed and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all actions and transactions whatsoever use and sign the said **ANNAMARY AUGUSTINO KOMIE** as my name in lieu of the former name of ANAMARY KOMIYE AND I hereby Authorise and Request all persons to designate and address me by such assumed name of **ANNAMARY AUGUSTINO KOMIE** , only .

I,the said ANNAMARY AUGUSTINO KOMIE, make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of the Oaths (Judicial Proceedings and Statutory Declarations)Act, 1966.

In Witness Whereof I have executed this Deed the 20th day of March 2023.

Signed at Mbinga by the said )
ANNAMARY AUGUSTINO KOMIE )
Who is known me personally this ..20 )
day of ......03...... 2023 )
Signature..........
Address..........
Qualification..........

DEPONENT



---

## KUPOTEA KWA CHETI



**PASKALINA ERASTO MIYUNGUA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. S4465-0010 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **QUEEN MARY'S SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/CHA/RB/48016/2023.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO...14....OF 2023**

**IN THEMATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HENRY WILLIAM BASS**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION BY EDITH WILLIAM BASS**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 23 day of June 2023.

Dated at Korogwe this 26 day of May, 2023.

DISTRICT COURT KOROGWE TANZANIA
DISTRICT COURT KOROGWE
RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**LUKUNGU INVESTMENT CO. LTD** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 104 DAN.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/184279/2023.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NASIBU MILIMO** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 875 CGB.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/184256/2023.**

---

**WTL**

WILCO TANZANIA LIMITED

**WILCO TANZANIA LIMITED**
[Company registration Number: **138842762**]

**RE: NOTICE OF VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY**

Notice is hereby given to the General Public that according to section 333 (b) of the Companies Act No.12 of 2002

Members of the Company through a Special Members meeting dated 31st December 2022 have voluntarily decided to Wind Up the Company. It was further resolved that JOSEPH JACOB MBOGO T/A ACME BUSINESS CONSULT be appointed as the Liquidator of the company. This notification is issued to all who have a claim against the Company.

**IRENE JOSEPH MAGESA**
COMPANY SECRETARY

PO Box 75 • Mwanhuzi • Tanzania
Phone: +255 27 297 0341

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(DISTRICT REGISTRY OF MOROGORO)**
**AT MOROGORO**
**LAND APPEAL NO. 8 OF 2023**
***(Arising from the Land Application No. 30 of 2018 From Morogoro District Land and the Housing Tribunal at Morogoro)***
**JAPHET MBOGO...............APPELLANT**
**VERSUS**
**JUMA A. TEMBO..................1ST RESPONDENT**
**DANIEL MCHOME ..........2ND RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

**TO DANIEL MCHOME**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on **5th day of June 2023 at 09:00 AM** at the High Court of Morogoro.

Your required to appear in person or through your Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and your directed to produce on that day all documents which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed to hear the Civil Case and pronounce judgment in your absence.

**GIVEN** under my **HAND AND SEAL** of the court this **25th day of May 2023**

DEPUTY REGISTRAR HIGH COURT MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDINA NELSON NDELWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 445 DXC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/184553/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GORDIAN ROGASIAN MSIGALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Suzuki **ESCUDO** yenye namba za usajili **T 486 APQ.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **DOD/CH/RB/179079/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN C. MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 726 CWT.** Chassis No. **LC6PCJBJ7M0021298.** Engine namba **152FM1AA3R001826.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/117488/2023.**

---

## TANGAZO LA NOTISI MDAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) kwa mdaiwa sugu Ndugu Moshi Ibrahim Mwippi wa Buguruni mtaa wa Mivinjeni wilaya ya Ilala – Dar Es Salaam .

Aliyekopa na kushindwa kulipa deni la mkopo, unatakiwa kulipa deni lako la mkopo unaodaiwa na Tujijenge ndani ya siku sitini (60). Hii ni baada ya kushindwa kulipa deni lako la mkopo kulingana masharti na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa (siku sitini).

Ikiwa ni pamoja na kuruhusu dalali kuuza mali zako zilizotumika kudhamini mkopo uliochukua.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0677045064**
**Au Email: HYPERLINK "mailto:tujijengetanzania@tujijenge.or.tz"**
**tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

---

**HATI YA KUITWA SHAURINI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WTA/85**

**BARAZA LA KATA MUTUKULA,**
**WILAYA YA MISSENYI**

**MADAI NA. 15 YA MWAKA 2023,**

**DHIDI YA KARISTI FELIX RUTWAZA**

**KWA CELINA EVALISTI KARISTI,**
**KITONGOJI MUTUKULA TOWN**

Unajulishwa kwamba shauri tajwa hapo juu litasikilizwa siku ya Alhamisi Tarehe 01 Mwezi wa 06 Mwaka 2023 saa 3:00 asubuhi katika ofisi ya kata Mutukula. Hivyo unatakiwa uwepo kwa ajili ya kujibu shtaka la mgogoro wa ndoa wakati wa kusikilizwa shauri hilo katika tarehe iliyotajwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Baraza la kata hii leo Tarehe 25 Mwezi 05 Mwaka 2023.

BARAZA LA USHURUHISHI KATA MUTUKULA. TAREHE
KATIBU WA BARAZA LA KATA

**KATIBU WA BARAZA LA KATA**
**MUTUKULA**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **GOSBERT HENERICO KIBANI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki yenye namba za usajili **MC457AAK.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/153250/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha KIHONDA Mkoa MOROGORO**
**Shauri la Madai / Ndoa Na. 50/2023**

**Jina la Mdai: SELEMAN ABILAH**
**Jina la Mdaiwa: THERESIA BUNGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya (18) ya kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: THERESIA BUNGA WA KIHONDA IDIVA MOROGORO**

**Kwa kuwa mdai / Wadai ameleta / Wameleta Madai yake / yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) MADAI YA PESA TSH. 2,250,000/=**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe **01 Mwezi 06 Mwaka 2023** Saa **3:00** Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyohusu madai hayo kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautoudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolwa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe **18/05/2023**

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA MOROGORO

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Biden: Sheria ya Ushoga Uganda ifutwe

**WASHINGTON,** Marekani

MUDA mfupi baada ya Rais Yoweri Museveni wa Uganda kutia saini kuanza kutumika kwa sheria mpya inayokataza mapenzi ya jinsia moja nchini mwake, Rais wa Marekani, Joe Biden, amekuja juu, akishutumu kwamba ni ukiukwaji wa haki za binadamu na kikwazo kwa maendeleo.

Mwanzoni mwa wiki hii, Rais Yoweri Museveni aliupitisha muswaada huo wenye adhabu kali dhidi ya watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja kuwa Sheria ya Ushoga ya Mwaka 2023, baada ya kufanyiwa marekebisho ambayo vipengele vingi vyenye msimamo mkali havikurekebishwa.

Kwa mujibu wa taarifa yake iliyotolewa baada ya sheria hiyo kupitishwa Uganda, Rais Biden alilaani hatua hiyo ya kupitishwa kwa muswada huo wa sheria wenye utata unaoharamisha mapenzi ya jinsia moja, unaotoa adhabu ya hadi miaka 10 jela na faini ya hadi Sh. milioni 10 za Uganda.

**Pia Bunge la Uganda kupitia ukurasa wake wa Twitter lilisema wabunge wamechukua hatua hiyo ili kulinda utamaduni na maadili ya taifa hilo.**

"Ninaungana na watu duniani kote wakiwamo watu wengi wa Uganda katika kutaka sheria hiyo ifutwe mara moja, hakuna mtu anayestahili kuishi kwa kuhofia maisha yake wakati wote au kufanyiwa vitendo vya ukatili na ubaguzi, ni makosa," alisema Biden.

Aliongeza kuwa Marekani itafanya tathmini ya athari za sheria hiyo katika nyanja zote za ushirikiano wa Marekani na Uganda, na kusema inaweza ikasababisha kuwekewa vikwazo kwa baadhi ya watu.

"Tunafikiria njia nyingine zaidi, ikijumuisha kuandaliwa kwa vikwazo na marufuku za kuingia Marekani dhidi ya mtu yoyote aliyehusika katika uvunjwaji mbaya wa haki za binadamu ama rushwa," alisema Biden.

Taarifa iliyochapishwa kupitia akaunti rasmi ya Twitter ya Rais wa Uganda ilieleza kuwa Museveni ameukubali muswada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja wa mwaka 2023, ambao rasmi utakuwa sheria ya kupambana na mapenzi ya jinsia moja.

Pia Bunge la Uganda kupitia ukurasa wake wa Twitter lilisema wabunge wamechukua hatua hiyo ili kulinda utamaduni na maadili ya taifa hilo.

Mwezi Machi mwaka huu, Rais huyo aliyeko madarakani kwa takriban miongo minne aliwaelezea mashoga kuwa ni wapotovu na ni mwenendo wa tabia unaokiuka maadili.

Mswaada huo ambao umekuwa sheria pia unawagusa watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja, wamiliki wa nyumba, hoteli, vyumba vya burudani, waandishi wa habari, watengenezaji filamu na wengineo.

Pia muswada huo unapendekeza adhabu kwa wanaoeneza habari za ushoga kwa kuchapisha vitabu na wafadhili watatozwa faini ya Sh. milioni 100 za Uganda, wanaomiliki vyumba vya kufanyia ushoga watahukumiwa miaka saba jela wakati wamiliki wa nyumba watakaokodisha kwa mashoga watahukumiwa mwaka mmoja gerezani.

Inaelezwa kuwa tangu muswada huo ulipofikishwa bungeni, watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja wamekuwa wakikamatwa, kufukuzwa na wenye nyumba za kupanga na matukio mengi ya vitisho, unyanyasaji, ghasia na ubaguzi dhidi yao. **VOA**

## Moscow yashambuliwa kwa mara ya kwanza

**MOSCOW,** Russia

MJI mkuu wa Russia, Moscow umekumbwa na mashambulizi ya ndege zisizo na rubani wakati Ukraine inajiandaa kuanza mashambulizi makubwa dhidi ya vikosi vya Russia.

Inaelezwa kuwa shambulizi hilo lilifanyika jana alfajiri na kwamba hayajawahi kushuhudiwa katika mji huo, huku msaidizi wa rais wa Ukraine akikanusha nchi hiyo kuhusika na mashambulio hayo yaliyolenga mji wa Moscow.

Wizara ya Ulinzi ya Russia iliilaumu Ukraine kwa mashambulio hayo ya ndege zisizo na rubani dhidi ya jiji la Moscow na maeneo jirani, ikibainishwa kuwa watu wawili wamejeruhiwa pamoja na kusababisha uharibifu mdogo katika baadhi ya majengo ya makazi ya watu.

Meya wa Jiji la Moscow, Sergei Sobyanin, alithibitisha kuwa raia wawili wamejeruhiwa katika mashambulizi hayo na kwamba wakazi ambao majengo yao yameharibiwa wamehamishwa kwa muda mfupi kutoka kwenye sehemu hiyo.

Inaelezwa kuwa majengo hayo yaliyoshambuliwa yako kusini magharibi ya mji mkuu wa Moscow kitongoji ambapo wanaishi watu wenye uwezo mkubwa kifedha karibu na katikati ya jiji la Moscow na karibu na mbuga, huku wakazi kadhaa mojawapo ya majengo yaliyopigwa wakisema walisikia milio isiyo ya kawaida.

Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema ndege nane zisizo na rubani zilitumika katika mashambulio hayo na kwamba mfumo wa ulinzi ulizuia ndege hizo zote kuleta maafa katika maeneo yaliyolengwa. **DW**



Rais wa Kenya, William Ruto, akiwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergeï Lavrov, alipozuru nchini humo juzi. **PICHA: REUTERS**

## Kenya na Russia kushirikiana kibiashara

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto, amesema nchi yake itaendelea kushirikiana na Russia na kwamba baada ya kukutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov walijadiliana namna bora ya kukuza biashara baina ya mataifa yao.

Hayo yalibainishwa jana kupitia ukurasa wa kijamii wa Twitter, wa ikulu ya rais wa Kenya.

Mwanzoni mwa wiki hii Waziri Lavrov, alifanya ziara ya kushtukiza nchini Kenya, ikielezwa kuwa alikutana na Rais Ruto na kufanya naye mazungumzo, na kwamba ziara hiyo inafanywa wakati Moscow ikitafuta uungwaji mkono zaidi na Afrika.

Vyanzo kutoka pande zote mbili vilisema mbali na kujadiliana kuhusu masuala ya kibiashara, kuimarisha diplomasia ya nchi hizo mbili na usalama, pia walizungumza kuhusu mzozo unaoendelea kati ya Russia na Ukraine.

Ziara ya Lavrov, ilitafsiriwa na wadadisi wa mambo kama njia moja ya kujaribu kufunika kile walichokiita mashimo yaliyoachwa wazi na mwenzake wa Ukraine, Dmytro Kuleba, ambaye juma lililopita alikuwa ziarani barani Afrika.

Aidha, inaelezwa kuwa hiyo sio ziara ya kwanza ya Lavrov barani Afrika, kwani mwaka uliopita na mwanzoni mwa mwaka huu alizuru mataifa kadhaa, wakati Russia ikijiandaa kuwa mwenyeji wa mkutano na viongozi wa Afrika utakaofanyika mjini Moscow kati ya Julai 26 hadi 29 mwaka huu. **RFI**

**Ziara ya Lavrov, ilitafsiriwa na wadadisi wa mambo kama njia moja ya kujaribu kufunika kile walichokiita mashimo yaliyoachwa wazi na mwenzake wa Ukraine, Dmytro Kuleba, ambaye juma lililopita alikuwa ziarani barani Afrika.**

# AFRICAN SPORTS HATARINI KUSHUKA TENA DARAJA

Na Adam Fungamwango

BENCHI la ufundi la klabu ya Azam limeanza kuupigia hesabu mchezo wao wa fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) dhidi ya Yanga kwa kupanga kuitumia michezo yao miwili ya ligi iliyobakia kama sehemu ya maandalizi kuelekea kwenye fainali hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kally Ongala, alisema kabla ya kucheza fainali hiyo wana michezo miwili ya kumalizia msimu na yote wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kukusanya alama zote sita kabla ya kuigeukia Yanga kwenye mchezo wa fainali.

**Azam FC watacheza mechi hizo mbili za mwisho kwenye ligi ambapo Juni 3 watakuwa ugenini kucheza na Coastal Union kabla ya kurejea Dar es Salaam kuumana na Polisi Tanzania Juni 9.**

Alisema michezo hiyo miwili itakuwa mwanzo wao wa maandalizi kuelekea kwenye mchezo wa fainali kombe la FA ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Tunatambua umuhimu wa kila mechi zilizopo mbele yetu tunafanya maandalizi mazuri kupata pointi pia mechi hizi mbili za kumaliza msimu itakuwa mwanzo wetu wa kujiandaa na mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho, tumeanza kuipigia hesabu mechi yetu ya fainali," alisema Ongala.

Aliongeza wanaandaa timu kwa ajili ya kumaliza vizuri Ligi Kuu kwa kukusanya pointi zote sita lakini kuiandaa timu kwa ajili ya mchezo wa fainali dhidi ya Yanga.

"Msimu huu haukuwa mzuri sana kwenye ligi, tumekosa ubingwa hivyo kombe pekee ambalo tupo kwenye mstari wa kuwania ni ili la Shirikisho, tunajipanga kuhakikisha tunafanikiwa kulipata ili tusitoke kapa msimu huu," alisema Ongala.

Alisema wanafanyia kazi udhaifu wao waliouona kwenye michezo iliyopita ili kuhakikisha wanakuwa kwenye kiwango kizuri kwenye mechi zilizopo mbele yao.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lumumba jijini Da res Salaam wakifanya mazoezi katika Viwanja vya Jakaya Kikwete jana baada ya muda wa masomo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Azam FC aipiga 'chabo' Yanga

Na Adam Fungamwango

MSEMAJI wa klabu ya Azam FC, Hasheem Ibwe, amesema kocha wao mpya Youssouph Dabo anaanda 'dozi' kwa ajili ya Yanga baada ya kocha huyo kuwafuatilia wapinzani wao hao kwenye mchezo wao wa fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USM Algers Jumapili iliyopita.

Ibwe amesema Dabo alikuwapo uwanjani kwenye mchezo huo ambao Yanga ililala kwa mabao 2-1 na kwa sasa anaandaa mbinu zitakazowapa ushindi kwenye mchezo wao wa Kombe la FA.

Azam itaumana na Yanga kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) itakayochezwa Juni 12 Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Kocha wetu ameanza kazi kuelekea mchezo wetu wa fainali Kombe la Shirikisho, kwa kuanzia Jumapili alikuwapo uwanjani kuwafuatilia Yanga, anaandaa dozi kamili itakayotufanya kutwaa ubingwa wa michuano hii," alisema Ibwe.

Ibwe alisema wanashukuru mpaka sasa hakuna mchezaji aliyeripotiwa kupata majeraha kitu kinachowapa imani kubwa ya kufanya vizuri kwenye mchezo huo wa fainali unaosubiriwa na mashabiki wengi wa soka nchini.

"Kuwa na kikosi kamili kutampa kocha wetu wigo mpana wa kupanga kikosi chake, maandalizi yanaendelea kuelekea kwenye mchezo huu, tunaamini mambo yataenda vizuri kama na kuondoka na ubingwa wa kombe la FA," alisema Ibwe.

Aidha, alisema pamoja na kuanza maandalizi kuelekea mchezo huo wa fainali pia wamejipanga vyema kuelekea kwenye michezo yao miwili ya mwisho ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union watakayocheza nayo Juni 6 Mkwakwani na ule dhidi ya Polisi Tanzania watakaocheza Juni 9 nyumbani.

"Michezo yote mitatu ni muhimu kwetu, lakini mchezo wa fainali ya FA na hii miwili ya ligi ina utofauti wake kwenye maandalizi, tunaendelea kujipanga lengo likiwa ni kupata ushindi kwenye mechi zote ili tumalize ligi vizuri lakini tuchukue ubingwa wa FA," alisema Ibwe.

## 'Softball' yaenda Japan kupambana

Na Saada Akida

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Wasichana wa mchezo wa 'Softball' kinaondoka nchini leo kuelekea Japan katika mashindano maalum ya dunia yatakayoanza kufanyika Juni 2 mpaka Juni 6, mwaka huu.

Tanzania ni nchi pekee iliyopata fursa ya kuwakilisha Bara la Afrika katika mashindano hayo yatakayohusisha pia nchi za Mexico, Marekani, China wenyeji Japan.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Baseball Softball Tanzania (TaBSA), Alpherio Nchimbi (pichani chini), alisema kuwa kikosi hicho kitawakilishwa na wachezaji 16 kutoka Tanzania bara na Zanzibar.

"Tanzania itakuwa inakabiliwa na michezo mitano katika mashindano haya ambayo yatatupa fursa kuonyesha vipaji vya wachezaji wetu na kupata nafasi ya kujitangaza kwa kuweza kupata timu katika mataifa mbalimbali," alisema Nchimbi.

Aidha, Ofisa Michezo Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Maguzu, aliwataka wachezaji kwenda kuonyesha uzalendo na kupambana hadi hatua ya mwisho na kurejea nchini na ushindi.

"Nawakabidhi bendera kwenda kuwakilisha nchi katika michuano hii mnayokwenda kushindana, lakini niwaombe viongozi mfanye mazungumzo na waandaaji ili kupata nafasi ya kushiriki wachezaji wenye ulemavu ili kutoa fursa kwa wote," alisema Maguzu.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdubakari Nachiwa, alisema amewaandaa wachezaji wake vizuri kiufundi, kimwili na kiakili na wataenda kupambana na kuitangaza nchi kwa kurudi na ubingwa.

"Tunajiamini na timu ipo vizuri, hakuna majeruhi ila kikubwa tunaomba wadau na Watanzania kutuunga mkono na kutuombea tufanye vizuri," alisema Nachiwa.



HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## KANE KUZUIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur imedhamiria kuzima majaribio ya Manchester United ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, msimu huu wa joto, huku mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy akigoma kumuuza kwa timu pinzani ya Ligi Kuu England. ***(Mirror)***

## MOUNT AWANIWA MAN

ERIK ten Hag ana imani kuwa anaweza kumshawishi kiungo wa kati wa Chelsea, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24 ajiunge na Manchester United kama sehemu ya maboresho ya kikosi chake kwenye usajili wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

## RICE ATAKIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich iko tayari kulipa pauni milioni 95 kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, huku timu hiyo ya Ujerumani ikiwa na nia ya kuipiku Arsenal katika kuinasa saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

## ODEGAARD AWINDWA

KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Arsenal na Norway, Martin Odegaard, 24. ***(Mail)***

## MADDISON AGOMBEWA

KLABU za Tottenham Hotspur, Newcastle na Arsenal ni miongoni mwa timu za Ligi Kuu England zinamtaka, James Maddison, 26, wa Leicester City. Kiungo huyo wa kati wa England anaweza kununuliwa kwa takribani pauni milioni 40. ***(Mirror)***

## POTTER ATAFUTWA

KLABU ya Crystal Palace imemtafuta kocha wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter, 48, kuziba nafasi ya kocha iliyo wazi, huku Nice pia ikimtaka Mwingereza huyo. (Footmercato)

## CARVALHO KWA MKOPO

LIVERPOOL imekataa ofa ya kudumu ya uhamisho kutoka nje ya nchi kwa kiungo mshambuliaji wa Ureno chini ya umri wa miaka 21, Fabio Carvalho, 20, huku klabu hiyo ya Merseyside ikifikiria kumtoa kwa mkopo tu mchezaji huyo. ***(Athletic)***

## WARD-PROWSE ATAKIWA

WEST Ham inaongoza katika mbio za kumnunua James Ward-Prowse, 28, huku Southampton wakisema thamani ya kiungo huyo wa kati wa England ni pauni milioni 40. ***(Sun)***

## BRUNO KUBAKI

KLABU ya Newcastle United ina imani kuwa kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes, 25, atasaini mkataba mpya pale St James' Park licha ya kutakiwa na Barcelona. (90Min)

## FIRMINO ASUBIRI OFA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Roberto Firmino, 31, ambaye ataondoka Liverpool msimu huu wa joto, anasubiri kuona kama atafaa kwenye mipango ya Real Madrid kabla ya kuchukua uamuzi wa kuhamia Hispania. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI AMTAKA MESSI

●●● Sijui ni mashaka gani anaweza kuwa nayo kuhusu kurejea msimu huu wa joto...

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez amesema alimwambia rais wa klabu, Joan Laporta kwamba angependa kuwa na Lionel Messi msimu ujao na akasema anazungumza na mchezaji mwenzake huyo wa zamani mara kwa mara kuhusu uwezekano wa kurejea katika timu hiyo.

**Messi mwenye umri wa miaka 35 aliondoka Barca miaka miwili iliyopita, lakini atapatikana kama mchezaji huru msimu huu mkataba wake na Paris Saint-Germain utakapokamilika.**

"Kuhusiana na kile ninachosimamia, upande wa mambo ya soka, hakuna shaka kwamba ikiwa Messi atarudi atatusaidia," alisema Xavi akiiambia Diario Sport alipoulizwa kama Messi kurudi kungekuwa na maana.

"Hilo nimeliweka wazi kwa Rais, hilo sina shaka hata moja kwa sababu bado ni mtu wa tofauti, bado ana njaa, ni mshindi na ni kiongozi.

"Hatuna timu yenye vipaji vya 2010, kwa mfano, Messi analeta nini, analeta kipaji. Ana uwezo wa kutoa pasi ya mwisho, kupiga mipira ya adhabu, kufunga mabao.

"Kwa sababu hiyo, kwangu hakuna shaka kwamba anaweza kuongeza mengi. Lakini inategemea yeye."

Xavi alisema licha ya kuzungumza na Messi, ambaye alicheza naye wakati wakiwa Barcelona, hajui anachofikiria mchezaji mwenzake huyo wa zamani kuhusu mustakabali wake kwa sasa.

Hapo awali ESPN ilifichua kuwa ataondoka PSG mkataba wake utakapomalizika Juni, huku pamoja na Barca, pia kuna nia kutoka kwa Saudi Arabia na Ligi Kuu ya soka ya Marekani.

"Ni vigumu kujiweka katika viatu vya mchezaji ambaye ameshinda yote," aliongeza Xavi.

"Sijui ni mashaka gani anaweza kuwa nayo kuhusu kurejea msimu huu wa joto.

"Labda anaweza kuwa na mashaka kwa sababu ni mradi mwingine sasa na kwa sababu wachezaji muhimu ambao alikuwa na uhusiano mzuri nao, kama Sergio Busquets na Jordi Alba, wanaondoka. Sijui, siko ndani ya kichwa chake.

"Kwa uhusiano nilionao naye nadhani nimekuwa wazi sana, mlango uko wazi kwake hapa inategemea na uamuzi wake binafsi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,120,4

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 31 MEI,01 NA 02 JUNI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/05/23 | 21:00 | Al Wehda vs AL Faiha | 2.61 | 3.51 | 2.49 |
| 02. 31/05/23 | 21:30 | Arab Contractors vs Ismaily SC | 2.31 | 2.86 | 3.31 |
| 03. 31/05/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Roma | 2.57 | 2.92 | 2.87 |
| 04. 01/06/23 | 01:00 | Fortaleza CE vs Palmeiras | 2.84 | 3.20 | 2.29 |
| 05. 01/06/23 | 02:30 | Inter Miami CF vs NY Red Bulls | 2.71 | 3.13 | 2.62 |
| 06. 01/06/23 | 03:30 | Corinthians vs Atletico Mineiro | 2.90 | 3.11 | 2.30 |
| 07. 01/06/23 | 19:00 | Haras EL Hodood vs Aswan | 3.22 | 2.86 | 2.35 |
| 08. 01/06/23 | 20:00 | Jonkopings Sodra vs Osters IF | 2.87 | 3.50 | 2.29 |
| 09. 01/06/23 | 21:00 | Vestmannaeyjar vs HK Kopavogs | 2.69 | 3.21 | 2.40 |
| 10. 01/06/23 | 22:15 | Fylkir vs KR Reykjavik | 2.74 | 3.31 | 2.31 |
| 11. 02/06/23 | 02:00 | Sarmiento Junin vs NewellS Old Boys | 2.69 | 2.74 | 2.74 |
| 12. 02/06/23 | 20:30 | Austria Lustenau vs TSV Hartberg | 2.55 | 3.33 | 2.39 |
| 13. 02/06/23 | 20:30 | Josko Ried vs Wolfsberger AC | 2.47 | 3.28 | 2.49 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TEN HAG: MAGUIRE RUKSA KUONDOKA

**MANCHESTER,** England

KOCHA Erik ten Hag amedokeza kuwa beki wake Harry Maguire huenda akaondoka Manchester United msimu huu wa joto ikiwa beki huyo ataamua kuwa hafurahishwi na ukosefu wa muda wa kucheza.

Nahodha huyo alicheza mechi 16 pekee za Ligi Kuu msimu huu na amekuwa na hatia ya makosa kadhaa ya hali ya juu hivi karibuni katika mechi ya mwezi uliopita ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla.


Ten Hag amekuwa akisifu ushawishi wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 - ambaye alijiunga mwaka 2018 kutoka Leicester kwa pauni milioni 80 ikiwa ni ada ya rekodi ya dunia kwa mlinzi na yuko chini ya mkataba hadi mwaka 2025.

Wakiwa fiti, Lisandro Martinez na Raphael Varane wamekuwa mshikamano wa beki wa kati wanaopendelewa zaidi katika kampeni ya kwanza ya bosi huyo wa zamani wa Ajax, huku Luke Shaw akiingia wakati mwingine.

Sasa kocha huyo ametoa pendekezo kali zaidi kwamba muda wa Maguire ndani ya United unaweza kufikia kikomo.

"Hakuna mtu ambaye angefurahishwa na hali hii," alisema Ten Hag katika mahojiano na The Times.

"Hayuko vilevile. Yeye hufundisha kila wakati kwa viwango bora kwa hiyo anaishughulikia hali hiyo vizuri na yuko katika namna hiyo na katika unahodha wake ni muhimu kwa kikosi, "Lakini ana ushindani mkubwa pale (katika beki wa kati) na Raphael Varane, ambaye ni mzuri."



# Bellingham mchezaji bora wa msimu

**DORTMUND,** Ujerumani

NYOTA Jude Bellingham amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa msimu wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Kiungo huyo wa kati wa England alishinda tuzo hiyo siku mbili tu baada ya klabu yake Borussia Dortmund kukosa taji dhidi ya Bayern Munich kwa tofauti ya mabao.

Bellingham mwenye umri wa miaka 19 amecheza mechi zaidi ya 130 tangu ajiunge na Dortmund kutoka Birmingham kwa zaidi ya pauni milioni 20 miaka mitatu iliyopita.

Baada ya kupokea tuzo hiyo, alisema: "Kila mwaka au nusu mwaka ambao nimecheza kwenye klabu, wajibu wangu katika timu umeongezeka.

"Lazima niendelee kuwa kila mahali kwenye uwanja na kujaribu niwezavyo kuchangia kwenda mbele na kujaribu kudhibiti michezo, kujaribu kutawala safu ya kiungo.

"Wachezaji wenzangu, makocha na wafanyakazi wamenisaidia kujiendeleza.

"Nilikuja kwenye klabu kama kijana mwenye kipaji, lakini nimeongeza vipengele kwenye mchezo wangu ambavyo vimenipeleka kweny kiwango kinachofuata," alisma.

Bellingham, ambaye at fikisha umri wa miaka 2 mwezi ujao, alikuwa nahodl wa Dortmund msimu huu r kuwa nahodha mwenye um mdogo zaidi kuwahi kutoke katika klabu hiyo na kufun mabao 14 katika mashindar yote.

Amekuwa akihusishwa vik li kutaka kuondoka Ujeruma msimu huu wa joto, huku Re Madrid wakiripotiwa kuo goza katika mbio za kuwan saini yake.

## HABARI MICHEZO

48,224/-

# SBL KUENDELEA KUDHAMINI LIGI KUU YA WANAWAKE BARA

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa 2022/23 wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara 'Serengeti Lite' ulifika ukingoni wiki mbili zilizopita, JKT Queens ikiibuka na ushindi dhidi ya Mkwawa Queens katika mechi ya kuamua bingwa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) ambao ni wadhamini wakuu wa ligi hiyo, imeahidi kuendelea kuwekeza katika ligi hiyo kama moja ya njia ya kuwawezesha wanawake ili kuongeza ujumuishwaji wa kundi hilo katika mpira wa miguu.

Kampuni hiyo imekuwa ikiwekeza katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara kupitia bia yake ya Serengeti Lite tangu mwaka 2018 baada ya kuingia mkataba wa kudhamini mashindano hayo na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

**Udhamini huo umefanya SBL kuwa kampuni ya kwanza kutoa udhamini katika soka la wanawake. Tangu kuanza kwake, ligi ya wanawake imeongeza mashabiki katika mpira wa miguu kitaifa.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Mawasiliano wa SBL, Rispa Hatibu, alisema SBL imekua ikiwekeza katika soka kwa muda mrefu, kuanzia udhamini wa timu ya taifa 'Taifa Stars' kabla ya kuongeza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara katika sehemu ya udhamini wake. Ni jitihada za kukuza soka nchini.

"SBL iko mstari wa mbele kusimamia ajenda ya ujumuishwaji, na hili tunalitekeleza katika shughuli zetu za kibiashara na hata tunapofanya uwekezaji katika miradi ya kijamii huwa tunazingatia suala la ujumuishwaji, hii ndio sababu tuliona umuhimu wa kutanua udhamini wetu kwenye soka mpaka kufikia soka la wanawake ili kuhakikisha wanawake pia wananufaika na uwekezaji wetu kwenye soka," alisema Hatibu.

Hatibu alisema SBL itaendelea kutoa sapoti kwa wanawake katika soka kupitia udhamini wa ligi ili kuchochea maendeleo ya michezo na kuwawezesha wanawake walio katika fani ya michezo. Pia itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuwezesha wanawake katika michezo.

SBL iliingia katika udhamini wa ligi hiyo mwaka 2018 kama sehemu ya ajenda yake ya ujumuishwaji, ikiwa na lengo la kuwawezesha wanawake katika fani ya michezo na kuwapa fursa ya kujipatia kipato kupitia michezo.

Kupitia udhamini huo wa SBL, jumla ya timu 14 zinazocheza ligi hiyo zimenufaika na udhamini huo zikiwamo, JKT Queens, Mkwawa Queens, Simba Queens, Yanga Princesses, Mapinduzi Queens, Tiger Queens and Mlandizi Queen.

## Simba yaanza mikakati 'Super League'

INATOKA UK. 24

alisema Ahmed.

Baada ya kukosa ubingwa wa Tanzania Bara kwa msimu miwili mfululizo, huku ikiishia robo fainali kwenye michuano ya kimataifa, wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa wakiwapigia kelele kwa viongozi wao kufanya usajili wa wachezaji wenye uwezo watakaowavusha walipofikia sasa.

Uongozi wa Simba tayari upo kwenye mchakato wa kusaka wachezaji wenye uwezo ili kuwasajili kujiandaa na msimu mpya.

Katika hatua nyingine, Ahmed amesema kocha wao msaidizi Juma Mgunda bado yuko sana ndani ya benchi hilo akisaidiana vizuri na bosi wake Roberto na wanatambua umuhimu na uwezo wa kocha huyo mzawa kwa kuwa ndani ya timu hiyo anaishi vizuri na wachezaji wa benchi zima la ufundi.

Kauli hiyo ya Ahmed imekuja siku chache baada ya kuzagaa taarifa zikimuhusisha kocha huyo kutimka ndani ya kikosi cha Simba.

"Mgunda yupo sana Simba, kutokuwapo hizi siku mbili katika mazoezi ni kwa sababu alikwenda kwao Tanga kwa ajili ya mapumziko mafupi na sasa amerejea na ameendelea na majukumu yake ndani ya kikosi cha timu yetu, wanaofikiri kuwa anaondoka watasubiri sana," alisema Ahmed.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Kanali mstaafu, Adbulrahman Kinana, akicheza gofu katika mashindano ya mchezo huo yaliofanyika viwanja Lugalo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Yanga SC yatanguliza*

INATOKA UKURASA 24

Yanga ambayo mchezo wa kwanza Uwanja wa Benjamin Mkapa ilikubali kipigo cha mabao 2-1, inahitaji ushindi wa lazima kwenye mchezo wa marudiano kuanzia mabao 2-0 kuweza kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/06/23 | 16:00 | KFUM Oslo vs Kristiansund BK | 2.48 | 3.30 | 2.31 |
| 02. 04/06/23 | 16:00 | Raufoss IL vs Fredrikstad FK | 2.70 | 3.10 | 2.23 |
| 03. 04/06/23 | 16:00 | Skeid Fotball vs Bryne FK | 2.17 | 3.20 | 2.75 |
| 04. 04/06/23 | 16:00 | AIK vs Kalmar FF | 2.13 | 3.00 | 3.00 |
| 05. 04/06/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Sarpsborg 08 | 2.60 | 3.05 | 2.35 |
| 06. 04/06/23 | 18:00 | Sandefjord Fotball vs Odds BK | 2.60 | 3.15 | 2.29 |
| 07. 04/06/23 | 18:00 | FC Nordsjaelland vs Viborg FF | 2.22 | 3.70 | 2.70 |
| 08. 04/06/23 | 18:30 | Plaza Colonia vs Cerro Largo FC | 2.39 | 2.95 | 2.65 |
| 09. 04/06/23 | 19:30 | KRC Genk vs Royal Antwerp FC | 2.26 | 3.30 | 2.55 |
| 10. 04/06/23 | 19:30 | RCD Mallorca vs Rayo Vallecano | 3.05 | 3.20 | 2.21 |
| 11. 04/06/237 | 19:30 | Villarreal CF vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.45 | 2.39 |
| 12. 04/06/23 | 20:15 | Viking FK vs Molde FK | 2.70 | 3.30 | 2.12 |
| 13. 04/06/23 | 22:00 | US Lecce vs Bologna FC | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 14. 04/06/23 | 22:00 | Real Betis Seville vs Valencia CF | 2.60 | 3.50 | 2.36 |
| 15. 04/06/23 | 22:00 | RC Celta de Vigo vs FC Barcelona | 2.75 | 3.45 | 2.29 |
| 16. 04/06/23 | 22:00 | Elche CF vs Cadiz CF | 2.50 | 3.40 | 2.55 |
| 17. 04/06/23 | 22:00 | Espanyol Barcelona vs UD Almeria | 2.75 | 3.75 | 2.19 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 31/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 10:30 | 1884 | Taian Tiankuang vs Sichuan Jiuniu | 5.99 | 3.98 | 1.47 |
| 10:30 | 4616 | Qingdao Red Lions vs Suzhou Dongwu | 4.78 | 3.69 | 1.61 |
| 12:00 | 5429 | Phu Tho FC-PVF vs Cong An Nhan Dan FC | 5.75 | 4.00 | 1.46 |
| 13:00 | 1669 | Hoang Anh Gia Lai vs TT Ha Noi | 3.40 | 3.45 | 1.90 |
| 13:00 | 2247 | Dong Tam Long AN vs BA Ria Vung Tau FC | 2.81 | 3.12 | 2.30 |
| 13:30 | 1723 | Urawa Red Diamonds vs Sanfrecce Hiroshima | 2.88 | 3.09 | 2.28 |
| 14:00 | 4202 | M. Nam Dinh vs Hong Linh HA Tinh FC | 1.91 | 3.34 | 3.49 |
| 15:15 | 3453 | Ho Chi Minh City vs SHB DA Nang | 2.26 | 3.24 | 2.78 |
| 16:00 | 1194 | Van Yerevan vs Alashkert Martuni | 4.98 | 3.78 | 1.58 |
| 16:00 | 2384 | Merani Martvili vs FC Norchi Dinamo Tbilisi | 1.84 | 3.52 | 3.67 |
| 16:00 | 5660 | Loko Tbilisi vs WIT Georgia | 1.69 | 3.85 | 4.00 |
| 18:00 | 1240 | Slovacko B vs FK Hodonin | 1.80 | 3.74 | 3.63 |
| 18:00 | 1629 | FC Spaeri vs Kolkheti Poti | 1.60 | 3.84 | 4.67 |
| 18:00 | 1793 | AC Oulu vs Haka | 2.08 | 3.31 | 3.16 |
| 18:00 | 1992 | Valmiera Fk/Bjss vs FS Metta/Lu | 1.27 | 4.90 | 6.60 |
| 18:00 | 2091 | RC Arbaa vs ASO Chlef | 1.96 | 2.95 | 3.98 |
| 18:00 | 2511 | MC Magra vs CR Belouizdad | 6.84 | 3.47 | 1.50 |
| 18:00 | 5909 | Paradou AC vs El Bayadh | 1.67 | 3.22 | 5.20 |
| 18:30 | 1682 | Ilves Tampere vs Kapa | 1.42 | 4.37 | 6.04 |
| 18:30 | 2259 | FC Jazz vs Vifk Vaasa | 1.64 | 3.77 | 4.44 |
| 18:30 | 2611 | MFK Vitkovice vs Unicov | 8.50 | 5.81 | 1.23 |
| 18:30 | 3522 | FC KTP vs IF Gnistan | 1.57 | 4.05 | 4.67 |
| 18:30 | 3546 | Japs vs EIF Ekenas | 2.05 | 3.58 | 3.01 |
| 18:30 | 5895 | JJK Jyvaskyla vs KuPS Kuopio | 11.45 | 5.41 | 1.21 |
| 19:00 | 1298 | National Bank vs El Daklyeh | 1.98 | 3.02 | 4.03 |
| 19:45 | 2702 | NAC Breda vs Emmen | 2.90 | 3.45 | 2.20 |
| 20:00 | 3833 | MC Oran vs HB Chelghoum Laid | 1.17 | 5.58 | 15.50 |
| 20:00 | 4417 | US Biskra vs CS Constantine | 3.10 | 2.74 | 2.42 |
| 20:00 | 4629 | ES Setif vs JS Kabylie | 1.92 | 2.99 | 4.08 |
| 20:00 | 5058 | Utsiktens BK vs Orebro SK | 2.28 | 3.30 | 3.04 |
| 20:00 | 5477 | Landskrona Bois vs Trelleborgs FF | 2.11 | 3.41 | 3.30 |
| 20:00 | 5752 | Eyupspor vs Bodrumspor | 1.92 | 3.34 | 3.44 |
| 20:00 | 5768 | Gefle IF vs GIF Sundsvall | 2.57 | 3.26 | 2.67 |
| 20:00 | 5891 | IK Brage vs Ostersunds | 2.28 | 3.30 | 3.04 |
| 20:30 | 1465 | Colombia U20 vs Slovakia U20 | 1.41 | 4.15 | 6.64 |
| 20:30 | 5742 | Brazil U20 vs Tunisia | 1.13 | 6.59 | 15.44 |
| 21:00 | 1354 | Al Nasr Riyadh vs Al Fateh (KSA) | 1.32 | 5.33 | 7.90 |
| 21:00 | 1984 | AL Adalh vs Al-Ettifaq | 1.72 | 3.91 | 4.28 |
| 21:00 | 2175 | Dhamk vs Al Shabab Riyadh | 4.37 | 4.10 | 1.67 |
| 21:00 | 4610 | Al Khaleej Club vs Abha | 1.65 | 3.93 | 4.78 |
| 21:00 | 4776 | Al Ittihad Jeddah vs AL Tai | 1.30 | 5.54 | 8.31 |
| 21:00 | 4803 | Al Wehda vs AL Faiha | 2.92 | 3.45 | 2.28 |
| 21:00 | 5451 | Al Taawon vs AL Baten | 1.53 | 4.38 | 5.34 |
| 21:00 | 5953 | Al Hilal Riyadh vs Al Raed Club | 1.27 | 5.78 | 8.99 |
| 21:30 | 1153 | Crotone vs Foggia | 2.02 | 3.13 | 3.38 |
| 21:30 | 2062 | Cesena vs Vicenza | 2.04 | 3.13 | 3.33 |
| 21:30 | 4762 | Virtus Entella vs Pescara Calcio | 2.03 | 3.24 | 3.24 |
| 21:30 | 5733 | Arab Contractors vs Ismaily SC | 2.37 | 2.81 | 3.26 |
| 21:30 | 5965 | Pordenone vs Calcio Lecco | 2.02 | 3.09 | 3.45 |
| 22:00 | 4363 | Sevilla FC vs Roma | 2.66 | 2.86 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Mei 31, 2023
Nipashe



## Ten Hag: Maguire ruksa kuondoka

UKURASA 22




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana (kushoto), akimkabidhi kipa wa Yanga, Metacha Mnata, Sh. milioni 20 zawadi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa bao lao walilofunga Jumapili iliyopita kwenye mchezo wa fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Yanga walifungwa mabao 2-1, (wa pili kushoto) ni rais wa timu hiyo, Hersi Said. **PICHA: BINZUBERY**

# Yanga SC yatanguliza mashushushu Algeria

**Na Saada Akida**

## ●●● Lengo kukwepa hujuma za Waarabu kuelekea mchezo wao wa...

YANGA imejipanga kukwepa 'hujuma' zozote wanazoweza kukutana nazo ugenini baada ya kutuma mashushushu kutangulia Algeria kuweka mambo sawa kabla ya kikosi cha timu hiyo kuhakiki jaenda.

**Wakati kikosi cha Yanga kikitarajia kuondoka nchini kesho, tayari uongozi wa timu hyo umeshawatuma viongozi wawili ambao tayari wapo Algeria wakiweka mambo sawa na kufuatilia nyendo za wapinzani wao hao.**

Inaelezwa maamuzi ya kutuma mashushushu hao Algeria ni mapendekezo ya kocha Nasreddine Nabi ambaye alipendekeza mratibu wa timu hiyo Hafidh Saleh na mtaalamu wa uchambuzi wa video wa timu hiyo Mtunisia Khalil Ben Youssef kutangulia kuweka mambo sawa.

Mratibu wa timu hiyo, Hafidh aliiambia Nipashe kutokea Algeria kuwa wamewasili nchini humo na tayari wameanza majukumu waliyotumwa.

Alisema moja ya majukumu yao ni kuhakikisha wanapata hoteli watakayofikia wachezaji na viongozi lakini pia kufahamu mapema uwanja watakaoutumia kwa mazoezi kuelekea kwenye mechi hiyo ya Juni 3.

"Hii mechi ni kubwa, nimekuja kuweka mazingira sawa kuhakikisha wachezaji hawapati shida wakifika, hali ya hewa ni ya kawaida iliyozoeleka kama ilivyo Dar es Salaam," alisema Mratibu huyo na kuongeza,

"Mpira wa Afrika una mambo mengi na hii ni fainali, kuja kwetu pia ni kuangalia namna ya kukwepa mitego yoyote ambayo wapinzani wetu wanaweza kutuwekea, lengo letu kwenye mchezo huu ni ushindi tu, tunataka wachezaji wetu akili yao iwe kwenye mchezo huu," alisema Hafidh.

Kwa upande wake, Kocha Nabi alisema amelazimika kutanguliza baadhi ya watu wake muhimu kwa kuwa anataka kuona wanafanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo huo ambao una umuhimu mkubwa kwao baada ya kupoteza mchezo wa kwanza.

"Nadhani suala kubwa kwetu kwa sasa ni mchezo huu, nataka wachezaji wangu waelekeza akili zao kwenye huu mchezo, tunaendelea na maandalizi kwa sababu kila mmoja anatambua na kujua tumekosea wapi hivyo tunahitaji kurekebisha kabla ya kuelekea Algeria kwa ajili ya mchezo wa marudiano, lakini kingine nataka timu ikifika Algeria isipate tabu yoyote, akili iwe kwenye mchezo, naamini tuliowatanguliza Algeria wataweka mambo sawa," alisema Nabi.

Nabi, alisema bado hawajakata tamaa ya kuukosa ubingwa kwa kuwa wana dakika nyingine 90 za kurekebisha mambo.

"Kufungwa kwetu nyumbani kumetusikitisha lakini bado hatujakata tamaa, tuna nafasi ya kufanya vizuri na kwenye mpira hakuna kinachoshindikana, tunaenda Algeria kwa lengo la kupambana na kubadilisha matokeo, hili linawezekana," alisema Nabi.

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yaanza mikakati 'Super League'

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema kwa sasa akili zao wanazielekeza kwenye michuano ya CAF ya Super League na tayari wameshaanza maandalizi ya michuano hiyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema jana kuwa, wakati viongozi, watu wa skauti na makocha wakiangalia wachezaji wa kuwasajili, mazoezi yanayofanyika sasa ni maandalizi ya Super League pamoja na msimu mpya wa Ligi Kuu wa 2023/2024.

"Tayari tumeshaanza maandalizi ya msimu ujao, haya yanayoendelea ni maandalizi ya ajili ya mashindano yajayo pamoja na ligi kwa sababu msimu mpya unaanza hivi karibuni, kama tulivyosikia msimu utaanza kwa nusu fainali ya Ngao ya Jamii itakayochezwa kwa mfumo wa timu nne msimu huu, kwa hiyo lazina tuanze maandalizi na michuano ya CAF msimu ujao itaanza mapema sana, tuko makini ndiyo maana tumeamua kuanza mipango mapema," alisema Ahmed.

Alisema pamoja na kwamba wachezaji wao wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi mbili za mwisho wa Ligi Kuu, lakini makocha wanatumia muda huo huo kuandaa kikosi cha msimu ujao na kuangalia wachezaji wa kuendelea kufanya nao kazi.

"Kikosi chetu kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi zetu mbili za mwisho, Polisi Tanzania Juni 6 na Coastal Union Juni 9, tangu ratiba ilivyosogezwa mbele kikosi kimeendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Mo Arena Bunju, dhamira yetu kushinda mechi zote mbili pamoja na kwamba sisi tumemaliza ligi, lakini mechi hizi zina thamani kubwa kwetu na mashabiki wetu,"

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >